DON MACLAFFERTY

# FUATA

Wakati wowote, Mahali popote, kwa gharama yoyote



# FUATA

## Wakati wowote, Mahali popote, kwa gharama yoyote

Hakimiliki © 2014
Katika Uanafunzi
Haki zote zimehifadhiwa
Chapa ya 2 na sahihisho mwaka 2015
Chapa ya 3 mwaka 2016
Chapa ya 4 na sahihisho la mwaka 2024

Isipokuwa imeoneshwa vinginevyo, aya za Biblia zimetolewa katika Biblia Maandiko Matakatifu, 1952 Union Version

Kimechapishwa na College Press
Collegedale, Tennessee

# YALIYOMO

Asante

Maelezo ya Mwandishi

Shairi “Wito”

1 Njoo

2 Fuata

3 Omba

4 Amini

5 Ondoka

6 Tumika

7 Penda

8 Ishi

9 Ngoja

10 Mwanafunzi-1

11 Mwanafunzi-2

12 Mwanafunzi-3

Changamoto Yangu kwa Uongozi wa Kikundi Kidogo

# Asante

Kwa Yesu, Yeye anayenipenda milele! Wewe ni Rafiki yangu wa karibu mno. Daima uko hapa pamoja nami. Ninatabaruku kitabu hiki Kwako.

Kwa April, mke wangu, mpenzi na rafiki. Nimezunguka kote ulimwenguni lakini kamwe sijaona mwanamke anayefanana na wewe. Wewe ni wa thamani sana kubwa kwangu. Umenitia moyo na kusimama nami wakati wa kuandika kitabu hiki. Upendo na utii wako kwa Mungu, kwangu na kwa watoto wetu ni faraja kubwa sana kwangu!

Kwa Jason, Julie, na Jessica—watoto wetu. Mungu amenifundisha kupitia upendo wenu, maswali yenu na safari za imani yenu. Maoni na mapendekezo yenu kuhusu kitabu hiki yameongeza thamani kubwa.

Kwa Merritt na Gail MacLafferty, wazazi wangu. Mlipanda mbegu za imani ndani ya moyo wangu kwa muda mrefu uliopita. Upendo wenu kila mmoja kwa mwenzake, kwangu na wadogo zangu na kwa Mungu daima unanibariki na kutia joto moyo wangu. Mawazo yenu yameboresha sana kitabu hiki.

Kwa Delain na Lydia Huggins. Upendo wenu kwa Mwumbaji na vyote alivyoviumba ulivuvia picha zote nzuri katika kitabu chote hiki.

Kwa David na Sharon Wheeler. Maombi yenu, uvumilivu wenu na uhariri makini uliyapa maneno yangu mbawa.

Kwa Jonathan Abrahams, Rick Ashodian, Dr. Kathy Beagles, Harry Bennett Sr., Harry na Marilyn Bennett, Dr. Jack Blanco, Gilbert Cangy, Curtis Cordwell, Luis Antonio de Menezes Dias, Dr. John Duge, Jocelyn Fay, Costin na Leah Jordache, Lynne Macias, Merritt na Gail MacLafferty, Hope Obermiller, Dr. Philip Saaman, Bonita Shields, Dr. Helder R. Cavalcanti Silva, na Helen Socol. Mmekuwa mduara wenye msaada wa usomaji wa kitabu hiki.

Kwa timu ya ajabu ya Uchapaji ya College. Mlifanya kazi kwa juhudi kubwa, haraka na kwa ufanisi. Mnafurahisha!

# Maelezo ya Mwandishi

Rafiki yangu, kikubwa kuliko mambo yote ulimwenguni, ninataka umjue Yesu! Siridhishwi na wewe kujua tu kweli kumhusu Yesu. Ninataka umjue Yesu kama Alivyo.

Yesu analeta mabadiliko chanya kila siku ya maisha yangu. Anabadilisha jinsi ninavyompenda mke wangu, jinsi ninavyowekeza katika watoto wetu, jinsi ninavyowatendea marafiki zangu na jinsi ninavyowapenda watu wenye matatizo. Ananipa tumaini ninapohisi kutokuwa na tumaini na kusudi la kuishi kila siku , kupenda na kuongoza.

Mara nyingi zisizohesabika amenisamehe nilipomkosea na nilipowakosea wengine. Msamaha Wake na upendo Wake usiobadilika unausukuma moyo wangu na unajaza moyo wangu kwa upendo mkubwa na shauku kubwa ya kumfuata. Sijapata mtu yeyote katika mabara yote sita ambayo nimeyatembelea anayenipenda kama Yesu!

Nina kualika kumtafuta Yesu katika kila sura na kumfuata popote anapokuongoza. Hatakuacha kamwe. Hatakukataa kamwe. Atakupenda milele. Kwa nini usimtambue Yeye aliye kwa ajili yako mwenyewe?

Kila sura itakusaidia kugundua ni nini maana ya kumfuata Yesu. Visa vinasimulia maisha ya watu waliomfuata Yesu katika karne ya kwanza. Kila kisa kinahitimishwa kwa maswali yafundishayo kukusaidi kutambua jinsi ya kumfuata Yesu katika karne ya 21.

Ili kunufaika zaidi kutokana na kitabu hiki, ninakupa haya mapendekezo unapoanza kila sura:

1. Mwombe Mungu akubariki unapoanza kila sura.
2. Furahia picha. Rafiki zangu, Delain na Lydia Huggins, walizipata picha hizi nzuri hasa hasa wakati wa matembezi yao katika misitu ya Tennessee.
3. Soma Maandiko yaliyopo upande unaotazamana na picha na tafakari jinsi uumbaji wa Mungu unavyoelezea Neno Lake.
4. Soma kisa kana kwamba ulikuwemo kabisa NDANI ya kisa.
5. Tafuta Nyakati za Malezi. Natamani kama ningekuwa kando yako unapogundua mambo mengi zaidi juu ya kumfuata Yesu. Furahia maswali yafundishayo ninayoshiriki nawe. Kwa nyongeza yanaweza kutumika kwa ajili ya kumfanya mtu mwingine kuwa mwanafunzi au kuoongezea vikundi vidogo.
6. Jizoeze kanuni hizi katika maisha yako tangu siku iyo hiyo.
7. Shiriki kile unachojifunza na mtu fulani ambaye atanufaika kwa kumfuata Yesu.

Tafadhali zingatia kuwa nimejumuisha mwongozo wa kikundi kidogo mwishoni mwa kila sura kwa wale miongoni mwenu ambao wangependa kuwaalika rafiki zenu waungane nanyi katika safari hii ya imani. Katika sura ya mwisho yenye kichwa cha habari “Uongozi wa Kikundi Kidogo” (ukurasa 110-113), nimejumuisha vidokezo vya nyongeza vya kufundishia kwa ajili ya kutumia kitabu hiki katika vikundi vidogo vidogo.

Ninaomba kuwa Mungu abariki safari yenu ya kumtumaini, kumfuata na kumshuhudia Yesu!



# WITO

Sikiliza–Je, unausikia?
Laini kama upepo mwanana, Angavu kama jua la
jioni lililopakwa rangi
Ukisihi  kama mnong'ono wa rafiki anayeaminiwa
Haiwezekani  kuupuuza unapokutana nao

Sauti hiyo hutoa uhuru, sio  shuruti,
Mwaliko ambao mara nyingi haufunguliwi kutoka
kwa Mtu Ambaye ahadi Zake hupita nyota katika
njia zake , Ambaye mawazo Yake  juu  yako huuzidi
mchanga

Sikiliza–Je, unausikia?
Ukiwaita vijana na wazee
Wawe wanaopendwa na wenye bahati
au wapweke na walioshindwa
Ukiwaita watafutaji wenye macho yaliyo wazi
wanaotafuta dhahabu
na yule ambaye amesahau kuota ndoto na ambaye
amejificha daima

Ukiwaamsha watoto wenye macho ya usingizi kwa
ajili ya jambo bora zaidi
Ukiwasihi mamilioni kufungua masikio yao
Wajitolee na kufungua milango ya mioyo yao
Kwa ajili ya matukio yasiyo na kikomo–amani ya
milele bila hofu
Sikiliza–Je, unausikia?
Ukitoa mwangwi katika zama zote bado unakuita
kweli
Wito wa kufuata ni kwa ajili yako

*na Julie MacLafferty*



*Mathayo 4:18-20*
*Marko 1:16-18*

# SURA YA KWANZA
# NJOO

***"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, name nitawapumzisha." Mathayo 11:28***

Akiwa ameunguzwa na jua. Mchanga katikati ya vidole. Misuli ikiwa imekaza wakati mikono yenye nguvu ikirusha wavu uliolowana karibu na ukingo wa ziwa. Wakati wavu unapopuliza hewani, unatua juu ya maji kwa weledi, unazama majini ambapo hakuna kina kirefu kwa ajili ya uvuvi wa asubuhi. Wavu unavutwa na kuingizwa katika mtumbwi, halafu unakusanywa na kutupwa tena majini. Mvuvi wa samaki anatabasamu wakati wavu unapopiga maji. Ni maisha mazuri– kutabirika, yenye faraja na huru. Anaijua kazi yake, kamba, mchanga na bahari...lakini nyakati zingine anashangaa ... je, ni haya tu?

Ni maisha. Huweka chakula mezani kwake kila siku. Anajua atakachokifanya kesho, siku inayofuata na siku elfu moja zinazokuja. Je! Kuna kitu kingine zaidi?

Petro amegubikwa na mawazo kiasi kwamba hamwoni Mwalimu akiwa anatembea kando kando ya bahari. Mwalimu anatembea akiwa peku kwenye ukingo wa maji.

Baadhi ya walimu hukaa katika madarasa makavu na hupumua hewa ya zamani. Baadhi husubiri wanafunzi wawatafute. Mwalimu huyu ni  wa tofauti. Anafundisha wakati upepo ukipiga uso Wake na mchanga ukiwa katikati ya vidole Vyake. Anakwenda watu wanapoishi.

Mwalimu anakwenda moja kwa moja hadi kwa Petro. Mvuvi anatazama, akiwa ameshangaa. Mwalimu anataka nini kwake? Je! Alikuwa katika matatizo?

Petro anaminya macho katika mwanga wa jua. Mwalimu anasema, “Njoo.” Mashaka yanajaa akilini mwake. Kwa nini mtu mkubwa kama huyu amwite yeye? Je, Mwalimu hakujua sifa yake, wakati wake uliopita, njia yake ya kutenda kabla ya kufikiri?

Mwalimu anatabasambu mbele ya Petro, anatikisa kichwa kuashiria kumkubali na anaendelea kutembea ufukweni bila kutazama nyuma. Nyavu zinateleza kutoka katika vidole vya Petro, zikianguka na kujirundika miguuni pake. Anatazama chungu kilichojaa samaki wanaoruka ruka.  Anakuja kwa Yesu Mwalimu kama alivyo—mvuvi wa kawaida, asiyekuwa na jambo lolote la ajabu akitafuta zaidi.

## Muda wa Mashauri

1. Kipi kinakufanya utake kumwendea  mtu mwingine? Kwa nini Petro alikuja kwa Yesu?

2. Soma Mathayo 4:18-20. Ni mambo gani yalimfanya Petro afae kwenda kwa Yesu? Yesu alimpa nini?

3. Soma Mathayo 11:28-30. Je! Yesu anatoa nini kwa wale wanaomwendea?

***Ninakualika uamue jinsi utakavyomjibu. Anakuita!***

4. Nina tumaini utakuja kama ulivyo. Njoo kwa Yesu ukiwa na matatizo yako, uraibu wako, misongo yako na hofu zako. Njoo Kwake ukiwa na hatia yako, aibu yako na uzito wa kumbukumbu za maumivu yako.

Mara nyingi sana tunafikiri kuwa inatupasa kusahihisha makosa katika maisha yetu kabla ya kuja kwa Yesu. Ninakusihi uje Kwake bila kujaribu kufanya jambo lolote kwanza. Atakuchukua kama ulivyo.

Jinsi Yesu anavyonikubali kama mtu, inanishangaza! Kufikiri kuwa ananijua, ndani na nje, pamoja na makosa yangu yote na kushindwa kwangu kote na bado ananiita nije Kwake–kunanijaza upendo kwa ajili Yake. Ruhusu moyo wako uguswe na jinsi anavyokupokea!

5. Kutatokea tofauti gani katika maisha yako ikiwa utakuja kwa Yesu kama ulivyo sasa hivi? Ninakualika uamue jinsi gani utamjibu. Anakuita!

CHANGAMO YA SIKU 7

**Yesu alikupata kama alivyompata Petro. Kila siku juma hili, ongea na Mungu kuhusu sehemu nzuri na mbaya ya siku yako.”**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura 1

**Ukaribisho** (dak.1) Mwambie kila mmoja jinsi ulivyo na furaha kuwaona. Mfanye kila mmoja katika kikundi ajisikie kukaribishwa, hata wale ambao wanaoenekana kutokupenda kuwepo hapo. Hakikisha kila mmoja anajumuishwa katika shughuliza kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Endesha aina fulani ya mchezo wa majina ambapo watu katika kikundi wanakariri majina ya kila  mmoja katika kikundi. Kwa mfano, mtu wa kwanza anataja jina lake na chakula anachokipendelea; mtu wa pili anasema jina la mtu wa kwanza na chakula chake pendwa na chakula  anachokipenda na kadhalika mpaka mwisho, mtu wa mwisho atalazimika kusema majina ya watu wote katika kikundi na vyakula pendwa vya wanakikundi wote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha ya mkono wa kushoto wa ukurasa

1. Uliza: Ni kwa jinsi gani kipepeo huonesha maisha yetu na kile ambacho Yesu anakitoa katika Mathayo 11:28? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kumtia moyo kila mtu.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa ili hadhira iweze kuhisi kuwa ipo  hapo kwa wakati huo!
Fikiria kuhusisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

**Wakati wa Malezi** (dak. 20) Soma Neno.  Jadilini mswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto katika ukurasa 4. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha

yako kinachofunua kile ambacho humanishwa na changamoto kwako binafsi. Usiogope kukabiliana na ushindi au kushindwa katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu kuiishi changamoto kwa siku saba zijazo kabla ya somo lijalo.

**Ombi** (dak. 2) Tumia muda huu kuwa kilele cha somo. Yesu anasema kuwa wakati atakapoondoka, Msaidizi mwingine, Mfariji angetumwa ili kuwasaidia (Yohana 14:16). Kwa ujasiri mwombe Mungu kwa ajili ya Mfariji, Roho Mtakatifu, atumwe kumsaidia kila mtu kufanya changamoto!



*Mathayo 9:9;*
*Marko 2:13-14*
*Luka 5:27-28*

# SURA YA PILI
# FUATA

***“Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.” Mathayo 4:19***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda kujibu swali hili: “Mungu alikusaidiaje katika kuifanyia kazi Changamoto ya Siku 7 kutoka katika sura ya mwisho?”*

Safu za sarafu, zikiwa zimepangwa katika mstari kama maaskari kwenye meza, zilimeremeta katika jua la Mediteraniani. Mathayo alipiga mwayo na kutabasamu mwenyewe. Faida yake katika siku hii ilipita faida ambayo watu wengi waliipata kwa mwezi. Alijinyoosha kama paka mvivu, akitafakari utajiri ambao angeweza kuukusanya katika miaka ijayo.

Alikuwa katika kilele cha ajira yake–ukusanyaji wa kodi. Wakati rafiki zake walipofikiria kuhusu pesa, walimfikiria yeye. Wakati jirani zake walipofikiri kuhusu mafanikio, walimfikiria kwa kijicho. Hakuwa mhitaji wa mambo mengi...isipokuwa kitu kimoja tu.

Alitamani kuwa sehemu ya kitu kilicho kikubwa

zaidi kuliko yeye mwenyewe, sababu ya kujitoa kwake k kwa mtu ambaye angeweza kumwamini.

Kwa ghafla Mwalimu alisimama kando ya meza ya Mathayo, akiziba mwanga unaomiminika kupitia katika mfuniko wa kibanda cha mtoza ushuru. Mwalimu alitabasamu. Wakati makuhani walipomtazama Mathayo walichukia, walinung'unika"mwenye dhambi" chini ya pumzi na walitazama upande mwingine walipompita katika mitaa.

Kanisa la wakati huo liliwanyanyapaa watu kama Mathayo. Aliwakilisha watu waliochukuliwa kuwa watu wa "daraja la chini" kidini. Alikuwa mdanganyifu na mshirika wa Rumi dhidi ya watu wake mwenyewe. Duara lake la marafiki liliundwa na watu waliokuwa na tabia inayotia mashaka. Lakini Yesu alikuwa akitabasamu kwa ajili yake!

Yesu alimwangalia Mathayo na alisema kile ambacho hakuna mwalimu mwingine angeweza kukisema, "Nifuate." Yesu alimwona Mathayo siyo tu kama alivyokuwa, bali kama vile ambavyo angeweza kuwa. Alimwona mfuasi mwaminifu.

Na huyo alikuwa ni yule Mathayo aliyetazama safu zake za sarafu zilizopangwa vizuri mezani. Alitazama kwa muda mrefu na kwa umakini pesa zake, kibanda chake na maisha yake ya raha – na akaondoka, kumfuata Yesu.

## Muda wa Mashauri

1. Kwanini umfuate Yesu? Chunguza hizi aya za Biblia kwa ajili ya sababu za kumfuata Yesu:

   Yohana 6:35

   Yohana 8:12

   Yohana 14:6

2. Soma Mathayo 9:9-13. Unafikiri Mathayo aliacha nini ili kumfuata Yesu? Unafikiri alipata nini?

3. Unamfuataje Yesu leo? Hapa kuna hatua chache za Kiutendaji:

(a) Soma 1 Yohana 2:6.

(b) Soma Zaburi 119:105. Neno la Mungu limeelezwaje? Unatakiwaje kuyatumia Maandiko ili yaweze kuongoza maisha yako?

***Rafiki, unaweza kuwa umemjua Yesu kwa miaka mingi, miezi michache au humjui kabisa. Nakualika kusoma Maandiko ujue jinsi ya kumfuata. Usiridhike tu na unayoyasikia yakisemwa na wengine kumhusu Yesu. Soma ukiwa na njaa ya kumjua na kumfuata wakati wote.***

4. Ni matokeo gani chanya yanaweza kutokea ikiwa tutamfuata Yesu kila siku?

## CHANGAMO YA SIKU 7

**Yesu anakuita kama alivyomwita Mathayo kutoka katika ukusanyaji wake wa kodi. Kila siku juma hili, mfuate Yesu mahali popote anapokuita.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa Ajili ya Sura 2

**Ukaribisho** (dak. 1) Shirikianeni kumwita kila mmoja kwa jina sahihi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Je, ungependa kuwa bilionea kwa siku moja au kuwa milionea kwa mwaka mmoja? Kwa nini?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililopita ukurasa wa 4:
*Yesu alikupata kama alivyompata Petro. Kila siku juma hili, ongea na Mungu kuhusu sehemu nzuri na mbaya za siku yako.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, uliongeaje na Mungu kuhusu sehemu nzuri na mbaya ya siku yako?
Mwalike kila mmoja kujiunga na mwingine kupata vikundi vya watu wawili wawili na waulizane ikiwa wailifanyia kazi changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Kumbusha wanafunzi watiane moyo wao kwa wao hata kama kuna mmojawapo hakuifanya kazi hiyo ya changamoto. Baada ya kila mmoja kuwa na dakika 1-2 za kuongea katika vikundi vya watu wawili wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au wawili ambao wangependa kushiriki na kundi lote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo upande wa kushoto wa ukurasa 9.
Uliza: Korongo wanarukaje? Ni kwa jinsi gani wanaonesha mfano wa Mathayo 4:19? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu atoe hekima na hamasa kwa kila mmoja aliyepo.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa ili hadhira yako iweze kujiona kimawazo kuwa ipo hapoe kwa muda huo! Fikiria kujumuisha wengine katika kundi lako wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (20 min.) Soma Neno. Jadilini maswali.

**Changamoto** (dak. 5). Soma changamoto ukurasa wa 12. Simulia kisa kutoka katika maisha yako kinaichofunua changamoto, je, inamaanisha nini kwako binafsi. Usiogope kufunua mafanikio na kushindwa kwako katika kuishi kulingana na changamoto hiyo. Mpe changamoto kila mtu ya kuiishi katika siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Uufanye wakati huu kuwa kilele cha somo. "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi" (Zek. 4:6). Kwa ujasiri mwombe Mungu amimine Roho Wake kwa kila mmoja!


Luka 6:12

# SURA YA TATU
# OMBA

***“ Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu.” Mathayo 26:41***

*Kabla hujaianza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: “Mungu alikusaidiaje kufanyia kazi Changamoto ya Siku 7 ya sura iliyopita?”*

Anga lilikuwa limejaa nyota, maelfu ya nyota ziking’aa kwa mwanga wao wote dhidi ya giza jeusi. Kulikuwa kimya, kimya kiasi ambacho mtu angeweza kuzisikia nyasi zikiunguruma katika upepo mwanana. Ulikuwa ni usiku kama maelfu ya usiku mtulivu kabla...isipokuwa...

Mlango wa zamani, wenye makovu wa nyumba ndogo katika mtaa pole pole ulifunguka. Sura ya kivuli kwa makusudi ilitoka nje na kuingia katika barabara ya vumbi, ikiepuka takataka za sherehe ya usiku uliopita. Mlevi alitambaa na kuvuka mtaa,

na mtu asiyekuwa na makazi alitetemeka katika baridi ya upepo wa usiku. Alirudi nyuma na kuweka koti lililokunjuliwa chini ya kichwa cha mlevi na kuweka blanketi ya zamani juu ya mtu asiyekuwa na makazi. Sura ile ilikuwa ya Mwalimu.

Mwalimu alikwenda mwendo mrefu na kupita safu za vibanda na kushika njia inayotumiwa sana inayoelekea juu ya kilima kidogo. Aliutazama mji wa nyumbani Kwake kwa muda mrefu, mrefu sana. Alishusha pumzi kwa nguvu na kushuka magotini Pake, akiwa bado anautazama mji, akipangusa machozi kutoka machoni  Pake.

Polepole alisimama na kutembea kuelekea upande wa pili wa kilima, mahali ambapo aliweza kuona nyota peke yake. Alitazama kwa muda mrefu na kwa makini nyota ambazo Yeye Mwenyewe aliziumba muda mrefu uliopita. Akinyosha mikono Yake mbinguni, Alisema yote yaliyokuwa moyoni Mwake. Nyakati zingine aliongea, halafu alitulia, akisikiliza. Alikuwa na maongezi mazito, yasiyokuwa na haraka, kama anaongea na rafiki wa karibu.

Anga lilibadilika na kuwa la bluu na baadaye lilipasuka na kuwa na mwonekano mpya wa rangi wakati Mwalimu  alipokuwa akishuka kutoka mlimani. Alimpungia mlevi, alitabasamu alipomwona mtu asiye kuwa na makazi, halafu alifungua mlango wa nyumba...na hadi siku nyingine.

## Muda wa Mashauri

1. Kwa nini unawekeza muda katika kuwasiliana na rafiki zako na familia yako? Kwa nini uwekeze katika kuwasiliana na Mungu kwa njia ya maombi?

2. Soma Marko 1:35. Yesu alikuwa na mazoea gani?

3. Unamwombaje Mungu? Hapa kuna hatua za kiutendaji:

(a) Omba kwa kumshiriki sha Mungu jinsi unavyohisi. Uwe mwaminifu. Daudi, katika Zaburi, anatupatia mifano mingi ya maombi ya uaminifu, ya moyo uliofunguka. Chunguza maombi ya Daudi kuona mambo aliyomwambia Mungu.

Zaburi 9:1, 2

Zaburi 13:1

Zaburi 18:1, 2

Zaburi 42:1, 2

Zaburi 51:7-12

(b) Omba ukitumia mada ambazo Yesu alizitumia wakati alipowapa wanafunzi Wake mfano katika Mathayo 6:9-13.

(c) Omba katika jina la Yesu. Tazama Yohana 15:16. Omba kwa ajili ya yale ambayo Yesu ameyaahidi. Nyakati nyingi tunaomba kwa ajili ya mambo ambayo tunayataka badala ya mambo ambayo Yesu ameyaahidi. Ikiwa tungeomba kwa ajili ya yale ambayo Yesu ameyaahidi, tungepokea majibu tofauti. Tazama 1 Yohana 5:14, 15.

(d) Omba kwa matarajio kuwa Atajibu. Tazama Zaburi 5:3; 91:15.

Namna ninavyoomba imeendelea kubadilika kwa kadiri miaka inavyokwenda. Maombi yangu ya awali yalikuwa rasmi sana, kama vile naongea na Mwenye Uhai anayeishi mbali, mbali sana kutoka kwangu. Katika ujana wangu nilisoma Zaburi na nilishtushwa kugundua jinsi Daudi alivyoongea na Mungu. Nilishangaa kuwa Daudi alizungumzia juu ya hasira yake, kukata tamaa kwake na kusema mashaka yake kwa Muumba wake! Maombi yake yalinipa changamoto kuongea na Mungu kama kuongea na rafiki Mtakatifu, na kuwa wazi kwa kile nilichokuwa nikikipitia katika maisha yangu.

Katika harakaharaka za siku, ni rahisi sana kutekwa mawazo na kusahau kuwa siku yangu yote inaweza kuwa ya maongezi na Mungu! Ni faraja kubwa kiasi gani kujua kuwa ninaweza kuongea na Mungu jambo lolote na wakati wowote.

Miaka michache iliyopita niligundua katika Neno la Mungu kile kinachoendelea kunibadilisha kwa nguvu kila siku. Ninasoma Isaya 50:4. Niligundua kuwa Mungu alitamani kuniamsha kila asubuhi ili anifundishe kama mwanafunzi Wake kutoka katika Neno Lake lililoandikwa na kwa njia ya maombi. Nilianza jaribio kwa kuomba kabla ya kulala usiku

ili Mungu aniamshe WAKATI WOWOTE kuja na na kutumia muda pamoja Naye.

Niligundua kuwa Mungu alikuwa tayari kusikiliza ombi langu kulingana na ahadi Yake katika Isaya 50:4. Asubuhi baada ya asubuhi ananiamsha nije na kumtafuta katika Maandiko na kusikia kile ambacho anataka kuniambia kuhusu maisha yangu.

Kama mtoto anayepata rafiki mpya na wa ajabu, nimemtambua upya Mungu kwa kuwa na muda usiokuwa na haraka kufurahia kile ambacho Anakisema katika Maandiko na kumngoja Yeye ili kusikia kile ambacho anakisema kupitia kwa Roho Wake anayeongea na moyo wangu. Mungu anayo mengi ya kutuambia tunapotulia bila haraka katika Uwepo Wake.

***Unaweza kuwa unafikiria, "Ninawezaje kujua ikiwa ninamsikia Mungu akiongea na moyo wangu?" Rafiki yangu, DAIMA zipime hisia zako na uelewa wako kwa njia ya Neno la Mungu lililoandikwa. Mungu KAMWE hatakuongoza katika njia ambayo inapingana na Neno Lake liliondikwa!***

4. Ni jambo gani litabadilika katika maisha yako ikiwa utaomba kama maongezi endelevu na Mungu muda wote kila siku?

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu alizungumza na Baba yake kama rafiki. Kila Siku katika juma hili, zungumza na Yesu Kwa uwazi kama ufanyavyo Kwa marafiki zako.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa Ajili ya Sura 3

**Ukaribisho** (dak. 1) Kutana na kila mmoja mlangoni na wasalimie kwa majina yao. Mfanye kila mmoja ajisikie kukaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Jifikirie unaungua katika nyumba ambayo huna njia ya kutoka nje. Utamwita nani kwanza na kwa nini? Utamwita nani wa pili na kwa nini?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililopita ukurasa 12:
*Yesu anakuita kama alivyomwita Mathayo kutoka katika utozaji wake wa kodi. Kila siku juma hili, mfuate Yesu mahali popote anapokuita.*
Uliza: Katika siku saba za mwisho, wapi Yesu alikuita? Uliitikiaje wito Wake?
Mwalike kila mmoja kuungana na mwingine kuunda timu ya watu wawili wawili na kila mmoja amwulize ikiwa aliifanyia kazi changamoto na mambo yalikwendaje. Wakumbushe wanafunzi watiane moyo wao kwa wao hata kama kuna mmoja hakuifanyia kazi changamoto. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 za kuongea katika makundi ya watu wawili wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au wawili ambaye angependa kushiriki na kundi lote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo upande wa mkono wa kushoto wa ukurasa 17.
Uliza: Kuchakuro anaonekana akifanya nini wakati huu? Yesu anawaelekeza wanafunzi Wake wafanye nini katika Mathayo 26:41? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kumtia moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo hadhira yako itajiona kuwa sehemu ya kisa hicho kwa muda huo!

Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadilini maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto katika ukarasa wa 22. Simulia kisa kutoka katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto kwako bianafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kushinda au kushindwa katika kuiishi changamoto. Mpatie changamoto kila mtu kuiishi changamoto katika siku saba kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo lako. Mungu anasema kuwa anapenda sana kutupatia Roho Mtakatifu kuliko baba anavyowapatia watoto wake vipawa vyema (Luka 11:13). Kwa ujasiri mwombe Mungu amwage Roho Mtakatifu juu ya wana kikundi ili awasaidie kufanya changamoto hii.


Mathayo 14:24-33

# SURA YA NNE
# AMINI

***"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi." Yohana 14:1***

*Kabla ya kuianza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Mungu alikusaidiaje kufanyia mazoezi Changamoto ya Siku 7 ya sura iliyopita?"*

Mwalimu alisema waondoke, kwa hiyo waliondoka – bila wao kupenda. Kwa mtazamo wa kiutendaji, huu ulikuwa wakati mbaya zaidi wa kuuacha umati wa watu. Mwalimu alikuwa ndiyo tu ameulisha umati wa watu elfu kwa mlo wa mchana wa mvulana mdogo. Wakati huo wanafunzi waliweza kuona fursa za kusisimua–kila mmoja alitaka kumfanya awe Mfalme! Walikuwa na kila kitu cha kupata ikiwa wangebaki, na kila kitu cha kupoteza kwa kuondoka.

Kwa kukijilazimisha, waliusukuma mtumbwi wa zamani, waliouzoea na kuuingiza ziwani. Watu kumi na mbili waliokata tamaa walitembea na kuvuka ukingo wa maji na kusukumana kuingia katika mtumbwi, wakiwa wameshangaa. Hakika Mwalimu hakutumia busara. Kwa nini awaondoe sasa?

Wakipiga kasia ili kuvuka ziwa, safari yao ya unyongonyevu ilishikwa na mkondo wa upepo. Wanaume walipumzika na kutabasamu upepo ulipochukua nafasi na kuingilia  kazi yao. Mawingu yaliyotawanyika yalikusanyika, yalijikusanya pamoja kama ngumi na kuwa meusi. Upepo ulivuma na kuyapiga matanga ya mtumbwi. Jua lilizama chini ya upeo wa macho na mawimbi yalirukia ndani ya mtumbwi. Pwani ilikuwa wapi?

Dhoruba iliupiga mtumbwi mdogo bila huruma. Ukiwa umepeperushwa na kurushwa na upepo, usiku ukawa mzito, mawimbi yalipiga juu ya mtumbwi, watu waliioonja hofu halisi: wote walikuwa wanakwenda kuzamishwa ndani ya maji!

Katika giza, mwanga wa radi unafunua jambo lisilowezekana–sura ya kutisha ilitembea kuelekea waliko juu ya maji! "Ni mzimu!" walipiga kelele. Hofu ilichoma kama kisu katika mioyo yao. Je, hii ilikuwa roho ya mauti—ikiashiria maangamizi yao?

Mtembea juu ya maji aligeukia upande wa mtumbwi. Alisema, "Jipeni moyo. Ni Mimi. Msiogope!" Wale kumi na mbili waliielewa sauti ile. Waliutambua uso. Alikuwa Mwalimu wao! Alikuwa Yesu.

Wanafunzi walikuwa na shauku ya Yesu kujiunga nao ndani  ya mtumbwi. Alikuwa amemfanya kipofu kuona na mtu aliyekufa  kuwa hai. Wakiwa Naye mtumbwini, wangekuwa salama.

Mtu mmoja alijaribu kuamini jambo lisilowezekana. Aliondoka mtumbwini na kujiunga na Yesu mahali pale Alipokuwa. Petro alipiga kelele akiongea na Mwalimu juu ya ngurumo ya upepo, "Bwana, ikiwa ni Wewe, niambie nije juu ya maji!" Petro anasimama, akaenda akipepesuka kuelekea katika ukingo wa mtumbwi. Mikono inayopiga huku na huku inajaribu kumvuta nyuma, na kumkalisha chini. Sauti ya maneno ya dhati inampa changamoto ya kubaki mahali alipo, asifanye tendo la kipumbavu na ashikilie kitu ambacho anaweza kukitumainia.

Maneno ya Mwalimu yanasikika kama sauti kali ya tarumbeta juu ya mawimbi, “Njoo!” Wanafunzi kumi na moja wanaangalia. Petro anaruka nje ya mtumbwi—na anaanza kutembea juu ya maji! Macho ya Petro yanamwangalia Yesu. Anatembea mahali ambapo hakuna mwanadamu wa kawaida aliwahi kutembea.

Lakini Petro anabadilisha mwelekeo wa macho na anatazama mawimbi yaliyorushwa na upepo. Akiwa ameondoa fokasi kwa Yesu, anatumbukia kwa ghafla kama  aliyevutwa na kuingizwa katika shimo la maji machafu. “Bwana, niokoe!” anapiga kelele. Mara moja Mwalimu ananyosha mkono na kumvuta na kumwezesha kusimama tena juu ya maji. Yesu anamwangalia machoni kwa makini na kumwuliza, “Ewe mwenye imani haba, kwa nini uliona shaka?”

Yesu anampandisha Petro katika mtumbwi. Dhoruba inanyamazishwa.  Ukimya unatawala juu ya uso wa bahari. Mawingu yanarudi nyuma. Matanga yanainama. Wale wanafunzi kumi na wawili, wakiwa na sauti zinazokwaruza na kwa mshangao, wanapumua na kutamka maneno, “Hakika Wewe ni Mwana wa Mungu!”

## Muda wa Malezi (Sehemu 1)

1. Fikiria juu ya mtu unayemwamini. Kwa nini unamwini?

2. Soma Mathayo 14:22-33. Kisa hiki kinakufundisha nini kuhusu kumwamini Yesu?

3. Unamwaminije Yesu? Hzi ni  hatua za kiutendaji za kukua katika kumwamini Yesu:

(a) Warumi 10:17 Soma Biblia. Imani yako itaongezeka.

(b) Marko 9:24 Mwombe Mungu akusaidie kutokuamini kwako.

(c) Yakobo 2:17; Yoshua 3:13-17 Unapoyajua mapenzi ya Mungu, yatekeleze!

4. Maisha yako yangefananaje kama ungemwamini Yesu kikamilifu?

CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu alikuwepo kwa ajili ya Petro alipizama kwenye maji. Kila Siku juma hili, mtumainie Kwa jambo fulani.**

## Muda wa Mashauri (Sehemu 2)

Gundua furaha na amani ya kumwamini Yesu kikamilifu kwa ajili ya maisha yako na mustakabali wako. Hapa kuna hatua tano za kumwamini Yesu kwa ajili ya maisha yako na uzima wa milele:

1. Soma Warumi 5:7, 8; 8:38, 39. Uwe na uhakika kuwa unapendwa na Mungu bila masharti.

2. Soma Warumi 3:23; 6:23. Uwe na hakika kuwa unamhitaji Yesu kama Mwokozi wako.

3. Soma Warumi 6:23 (sehemu ya mwisho); Yohana 3:16;  Efe. 2:8, 9.

Uwe na hakika kuwa Yesu anakupatia uzima wa milele kama zawadi unapomwamini kama Mwokozi wako.

4. Soma 1 Yohana 1:9 Uwe na hakika kuwa Yesu anakupatia moyo safi.

5. Soma Ufunuo 3:20 Uwe na hakika kuwa Yesu anakuja katika maisha yako unaposalimisha Kwake utawala wa maisha yako na kumwalika aje na kuwa UZIMA wako.

Rafiki, ninakumbuka wakati nilipokuwa sina amani na Mungu kuhusu wokovu wangu. Nilikuwa na wasiwasi kuhusu ikiwa nilikuwa mwema kiasi cha kutosha. Nilifokasi zaidi kwa kile nilichokuwa nikikifanya badala ya kile ambacho Yesu amekifanya na anakifanya kwa ajili yangu.

Nilipokuwa shule ya sekondari mtu fulani alitumia muda kunisaidia kumwamini Yesu na kile ambacho alikifanya kwa ajili yangu juu ya msalaba. Nilioneshwa aya za Biblia ambazo nimeshiriki nawe sasa hivi. Niliposoma 1 Yohana 5:13, Mungu alinifanya nifurahi sana! Nilifurahi kutambua kuwa ningeweza KUJUA kuwa nilikuwa na uzima wa milele kwa njia ya Yesu!

Kuwa na uhakika kuwa Yesu amenipatia zawadi bure ya wokovu kumenijaza upendo mwingi sana kwa ajili Yake. Kwa sababu ya kile alichofanya kwa ajili yangu, ninataka nimtumikie. Ninataka kumtii. Amenipatia zaidi ya ninavyoweza kumpa Yeye!

Rafiki, mshukuru Yesu kwa kukupenda jinsi ulivyo! Hakuna kitu chochote kinachoweza kukutenga na upendo Wake. Upendo Wake hauna masharti. Anakupenda sana kiasi ambacho atakusaidia uwe jinsi unavyoweza kuwa! Kwa hiyo mkimbilie.

***Mshukuru Yesu kwa kufa badala yako na kuchukua adhabu ya dhambi zako. Mwambie kuwa unaamini kwamba kile alichokifanya kwa ajili yako ni zawadi unayoipokea.***

Mwombe Yesu akusamehe dhambi zako. Atafanya hivyo! Atakupatia moyo mpya na mwanzo mpya. Mwalike Yesu sasa hivi aje katika maisha yako na awe Uzima wako.

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu alikufa ili kukupatia wokovu . Juma hili, mshukuru kila siku kwa ajili ya wokovu wako. Shiriki habari hii njema na mtu mwingine.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa Sura ya 4, sehemu ya 1

**Ukaribisho** (dak. 1) Mwambie kila mmoja jinsi ulivyo na furaha kuwaona.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Fikiria kuwa umeshinda tiketi iliyolipiwa gharama zote za safari ya kwenda mahali popote Ulaya. Ni uzoefu gani mmoja ungeupenda zaidi kuwa nao?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo la 22: *Yesu aliongea na Baba Yake kama kwa Rafiki Yake. Kila siku juma hili, ongea na Yesu wazi wazi kama unavyoongea na rafiki zako.*
Omba: Katika siku saba zilizopita, ni kwa jinsi gani namna ulivyoongea na Yesu kunalingana na jinsi uanvyoongea na rafiki zako?
Mwalike kila mmoja aungane na mwenzake ili kuunda vikundi vya watu wawiliwawili na waulizane jinsi walivyoitekeleza changamoto na jinsi zoezi lilivyokwenda. Wakumbushe wanafunzi watiane moyo hata kama kuna mtu hakuifanya changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja kuwa na dakika 1-2 za kujadiliana katika vikundi vya watu wawili wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili walio tayari kushiriki uzoefu wao na kundi zima.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo upande wa kushoto wa ukurasa 27. Uliza: Bata huyu anahitaji kujua nini kabla hajatua juu ya maji asiyoyajua? Ni kwa namna gani uzoefu huo wa bata unaelezea Yohana 14:1? Jadili.

**Ombi** (dk. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu afungue mioyo ili msikie na kutii kile ambacho Mungu anawaambia.

**Kisa** (dk. 5) Soma kisa kwa namna ambayo wasikilizaji wako watajiona kuwa wapo hapo wakati huo katika kisa! Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

**Muda wa Malezi** (dk. 20) Soma Neno. Jadilini maswali.

**Changamoto** (dk. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 31. Simulia kisa kifupi katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto kwako mwenyewe binafsi. Usiogope kuwa halisi kuhusu ushindi wako na kushindwa kwako katika kuishi changamoto. Mpe changamoto kila mmoja kuiishi changamoto kwa siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo. Yohana 7:37-39 inasema ikiwa tuna kiu, Mungu atatunywesha na kutufanya "mito ya maji yaliyo hai." Kwa ujasiri mwombe Mungu amwage Roho Wake ili kumsaidia kila moja kuwa huo "mto wa maji yalio hai"—chanzo cha faraja—kwa mtu fulani leo!

## Mwongozo Kikundi Kidogo wa Sura 4, sehemu ya 2

**Ukaribisho** (dak. 1) Mwambie kila mtu jinsi ulivyo na furaha kumwona.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ikiwa ungekuwa Rais wa Tanzania kwa siku moja, ni nini kingekuwa kipaumbele chako cha juu kabisa kuliko vyote?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililopita ukurasa wa 31:
*Yesu alikuwa karibu wakati Petro alipozama majini. Kila siku juma hili, mtumaini Yesu kwa ajili ya shida inayokusibu.*
Uliza: katika siku saba zilizopita, ulifanya nini kumtumaini Yesu kwa ajili ya matatizo yako? Mwalike kila mmoja kujiunga na mwenzake na kuunda vikundi vya watu wawili wawili na waulizane ikiwa walifanya changamoto hiyo na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja awe anamtia moyo mwenzake hata kama hakufanya changamoto. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 kujadili na mwenzake katika vikundi vya watu wawili wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili ambao wanaweza kuongea na kundi zima.

**Uliza** (dak. 3) Ni mtu gani mmoja unaweza kumwamini ikiwa maisha yako yanahitaji kumtegemea mtu? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu afungue mioyo na akili kwa ajili ya kile ambacho anamwambia kila mtu siku ya leo.

**Muda wa Malezi** (Sehemu 2) (dak. 25) Soma Neno. Jadilini maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto katika ukurasa wa 34. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua kile ambacho changamoto inamaanisha kwako wewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli juu ya kushinda kwako au kushindwa kwako katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu kuiishi changamoto kwa siku saba zinazofuata kabla ya somo linalofuata.

**Omba** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema anataka kutupatia haki, amani na furaha katika Roho Mtakatifu (Warumi 14:17). Kwa ujasiri mwombe Mungu amwage Roho Mtakatifu na kuwapa watu haki , amani, na furaha wanapomfuta Yesu njia yote, na wanapoendelea kukua katika uhusiano Naye!


Yohana 8:3-11

# SURA YA TANO
# ONDOKA

***"Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata."***
***Mathayo 4:20***

*Kabla ya kuianza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusaidia kufanyia mazoezi Changamoto ya Siku 7ya sura iliyopita?"*

Nguo zimechanika, nywele zake ndefu siyo nadhifu, mwanamke anangoja akiwa na hofu katika miguu ya Mwalimu. Kwa nini hakumchagua kwa makini mteja wake wa mwisho? Kwa nini alimwamini mtu ambaye sasa anamsaliti?

Viongozi mahalia walikuwa wamemvizia na kumkamata wakati usiofaa kabisa. Wanamwacha mwanaume aende akiwa huru. Walimkokota mwanamke kwa Mwalimu. Walitaka wamtumie kama chambo cha kumtega Mwalimu katika hukumu Yake juu ya mwanamke. Sheria ya watu wao ilisema alipaswa apigwe kwa mawe. Sheria ya Kirumi ilisema Wayahudi wasingemwua mtu bila ruhusa yao. Cho chote ambacho angekisema, wangemshitaki Mwalimu kwa kuvunja sheria mojawapo.

Alikuwa mzuri katika taaluma yake. Wanaume walivutwa na uzuri wake wa sura na walilipa fedha nyingi kwa ajili ya usiku pamoja naye. Alihisi kuwa mtawala. Alipata fedha nyingi. Alikuwa katika safari yenye kasi ya mafanikio. Daima alikuwa akijiambia kuwa angeacha maisha ya aina ile kesho, lakini sauti ya kugongwa mlango, na minong'ono ya ahadi za fedha daima vilimwingiza katika majaribu. "Sasa," alifikiri, "nitalipa kwa uhai wangu."

Mwalimu alimwangalia mwanamke anayetetemeka akiwa miguuni Pake. Kwa makini Alitathmini mandhari yote. Nyuso za kujihesabia haki za viongozi. Chuki yao dhidi Yake katika macho yao. Ukatili wao dhidi ya mwanamke.

Alipiga magoti katika mavumbi na akaanza kuandika kwa kidole Chake. Kwa udadisi, viongozi walisogea karibu, wakiwa na shauku ya kuua. Walipoona Alichokiandika, walijiona kuliko walivyowahi kujiona kabla. Washitaki walibadilika na kuwa washitakiwa.

Mawe yaliponyoka na kudondoka kutoka katika mikono yao walipokuwa wakitembea na kutawanyika.

Ndani ya muda mfupi Mwalimu alibaki na mwanamke peke yake. "Na mimi sikuhukumu. Nenda na usitende dhambi tena," Alisema.

Kungekuwepo na vita zaidi kwa ajili ya roho yake katika siku za mbele alipopambana na uwezekano wa ikiwa atayaacha yote aliyoyajua. Mwalimu alimpenda kuliko mtu mwingine yeyote alivyowahi kumpenda. Alimthamini kama mtu, binti wa Mfalme. Alimpa kile ambacho hakuna mtu alikuwa amewahi kumpa—heshima yake binafsi. Kwa hiyo aliachana na maisha yake ya zamani. Aliacha kila kitu nyuma na kumfuata Mtu ambaye asingemwacha kamwe.

## Muda wa Mashauri

1. Fikiria wakati uliponufaika kwa kuacha kitu fulani. Kwa nini ulikiacha?

2. Soma Yohana 8:1-11. Yesu alimwalika mwanamke kuacha nini? Soma Mathayo 16:24-26. Yesu ana matarajio gani kwa wanafunzi Wake?

3. Ni kwa jinsi gani unaacha kitu chenye madhara unachokipenda? Zifuatazo ni baadhi ya hatua za kiutendaji:

(a) Soma 1 Yohana 1:9. Ungama kwa Mungu na kwa rafiki zako kuwa umetenda maovu na unataka kubadilika. Pokea msamaha wa Mungu na msamaha wa wengine ikiwa inahitajika.

(b) Soma Ezekieli 36:26, 27. Mwombe Mungu akupe moyo mpya na amtume Roho Mtakatifu akupe nguvu ya kutamani mambo mema. Jisalimishe kwa Mungu.

(c) Soma Matendo 2:38. Geuka na uachane na kile unachokijua kuwa ni kosa.

(d) Mwalike rafiki unayemwamini awe mwenzako katika maombi akuwajibishe kila siku ili uwe mwaminifu kwa uamuzi wako. Tazama Wagalatia 6:2.

(e) Dai ahadi za Mungu. Tazama Wafilipi 4:6, 7, 13, 19.

***Jitenge na marafiki na mazingira yaliyokuhamasisha kwenda katika njia potofu. Badilisha njia potofu kwa kitu kinachotoa uzima kutoka kwa Mungu. Tazama 2 Timotheo 2:22.***

4. Fikiria kitu fulani katika maisha yako kinachokutenga na Yesu. Ni matokeo gani yangekuwa chanya katika maisha yako ikiwa utachagua kukiacha leo?

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu alitoa tumaini kwa mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi. Aliachana na maisha ya zamani. Kila siku juma hili, na upendo Wake ukikutia nguvu, acha chochote kitakacho hafifisha uhusiano wako Naye.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo Kwa ajili ya sura ya 5

**Ukaribisho** (dak. 1) Mkaribishe kila mmoja mlangoni na kumsalimia kwa jina. Mfanye kila mmoja kujisikia kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Lini na wapi katika maisha yako ulijisikia kutokuwa na wasiwasi na kuvurugwa?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto kutoka somo la mwisho ukurasa wa 34:
*Yesu alikufa ili kuthibitisha wokovu wako. Juma hili, mshukuru kila siku kwa ajili ya wokovu wako. Shiriki habari hii njema na mtu mwingine.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, ulimshukuru Yesu kila siku kwa ajili ya wokovu wako? Ulishiriki habari hii njema na nani?
Mwalike kila mmoja ashirikiane na mtu mwingine ili kuunda vikundi vya watu wawili wawili na kila mmoja amwulize mwenzake jinsi alivyoifanya changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja amtie moyo mwenzake hata kama mtu huyo hakufanya changamoto hiyo. Wakati kila mmoja ametumia dakika 1-2 kuongea na mwenzake katika vikundi vya watu wawili wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili wangependa kushiriki uzoefu wao na kikundi chote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyoko kushoto ukurasa wa 41. Uliza: Unafikiri mwewe anaacha nini? Picha hii inaoneshaje kile wanafuzi walichofanya katika Mathayo 4:20? Jadili.

**Ombi** (dk. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kuweka hamasa kwa kila moyo.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo wasikilizaji wanajiona kuwa sehemu ya kisa hicho kwa wakati huo! Fikiria kujumuisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 45. Simulia kisa kifupi katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto kwako mwenyewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusu kushinda na kushindwa katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu aishi changamoto kwa siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema atamwaga upendo Wake katika mioyo yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu (Rum. 5:5). Kwa ujasiri omba kuwa Roho Mtakatifu ajaze mioyo ya washiriki kwa upendo wanapofanya changamoto.

# *Yohana 13:1-9*



# SURA YA SITA
# TUMIKA

***"Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." Marko 10:45***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Mungu alikusaidiaje kufanyia kazi Changamoto ya Siku 7 kutoka katika sura iliyopita?"*

Chumba kilionekana kuwa mateso kwa wanafunzi kumi na mbili. Lakini haikuwa joto au unyevunyevu ambao ulikuwa tatizo–ilikuwa tarajio lisilotamkwa kuwa kitu fulani kilihitajika kufanywa na mtu fulani ambaye si wao.

Makapu ya mkate mpya na majagi ya sharubati ya zabibu vilijaza sehemu kubwa ya meza. Beseni la maji safi lilisubiri karibu na mitungi miwili ya mawe ya maji na kitambaa kilichokunjwa kwa unadhifu kando yake. Kilichokosekana jioni ile yenye joto la kadiri  ilikuwa mtumishi wa kuleta maji na

kitambaa na kuosha zile jozi kumi na tatu za miguu. Ni hakika, mmoja wao alipaswa kujitokeza. Wafuasi wa Mwalimu kila mmoja alikuwa na wazo la nani

alipaswa kujishusha. Wale waliokuwa watu wazima walifikiri kuwa walio vijana zaidi miongoni mwao ndiyo wangejitokeza. Wageni walijihisi walikuwa sawa na wenzao katika kundi. Kwa hiyo kila mmoja alisubiri, akikataa kutumika.

Kimya kimya Mwalimu alisimama na kutembea katikati ya chumba. Kwa hiari Yake Mwenyewe alivua koti Lake, akalikunja na kuliweka pembeni. Alijizungushia kitambaa kikubwa katika kiuno Chake na aliinama kuchukua beseni la maji. Alikwenda kwa mmoja wa wafusi Wake, akapiga magoti na kumwosha nyayo zake.

Kwa miaka mingi mikono migumu ya Mwalimu ilishika nyundo, misumari na mbao zinazokwaruza. Sasa ilishika nyayo zenye vumbi za wafuasi Wake. Mmoja baada ya mwingine, aliosha nyayo za wafuasi Wake na kuzikausha kwa kitambaa Chake. Kwa kurudia-rudia alipaswa kumwaga maji machafu na kuweka maji safi katika beseni.

Kila mmoja alitazama.

Mwalimu alikaa chini kula. Nyayo za kila mmoja zilikuwa safi, isipokuwa Yake. Hakuna aliyemhudumia. Hakuhisi chuki. Alikuwa ametumika... na hilo ndilo lilikuwa jambo muhimu Kwake.

## Muda wa Mashauri

1. Fikiria wakati ambapo mtu fulani alikuhudumia mahitaji yako bila ubinafsi wowote. Ni kwa jinsi gani tendo lao la ukarimu lilikugusa? Fikiria wakati ulipomtumikia mtu kwa mahitaji fulani bila wewe kupata manufaa yoyote.

***Kwa nini huduma isiyokuwa na ubinafsi inapaswa kuwa sehemu ya maisha yako ya kila siku?***

2. Soma Yohana 13:1-20. Yesu alifundisha nini kuhusu kuwatumikia wengine kwa mfano Wake? Gundua ni makundi gani ya watu Mungu hutuita kuwatumikia:

   Isaya 1:17

   Yeremia 7:6

   Yeremia 22:3

   Yakobo 1:27

4. Kungekuwa na matokeo gani ikiwa kwa kudhamiria kabisa ungehudumia mahitaji ya yatima, wajane, wageni na ma

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu aliwatumikia wanafunzi Wake. Kila siku juma hili, tafuta njia mahususi za kuwatumikia yatima, wajane, wageni, maskini au yeyote aliye na uhitaji.**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 6

**Ukaribisho** (dak. 1) Mkaribishe kila mmoja mlangoni na msalimie kwa jina. Mfanye kila mmoja kuhisi kukaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ni nani aliwahi kukuhudumia vizuri na kukufanya ujisikie kuwa umejaliwa?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo la mwisho ukurasa wa 45:
*Yesu alitoa tumaini kwa mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi. Aliacha maisha yake ya zamani nyuma. Kila siku juma kila, ukiwa na upendo Wake unapokutia nguvu, uache kitu chochote kinachoweza kuvuruga uhusiano wako Naye.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, ni kitu gani ambacho Yesu alikupa nguvu kuachana nacho? Mwalike kila mmoja akae na mwenzake waunde timu ya watu wawili-wawili na waulizane ikiwa walifanya changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja kumtia moyo mwenzake hata kama hakufanya changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja kuwa na dakika 1-2 za kuongea, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili wanaopenda kushiriki uzoefu wao na kundi zima.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyoko mkono wa kushoto ukurasa wa 49. Uliza: Ni manufaa gani nyuki huleta kwa ua linalochanua? Ni kwa jinsi gani hutoa picha ya kile ambacho Yesu hutufanyia, kama ilivyoelezwa katika Marko 10:45? Jadili.

**Omba** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kumtia moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo hadhira yako inaweza kujiona kuwa sehemu katika

kisa hicho kwa wakati huo! Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi chako wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 52. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua nini maana ya changamoto hii kwako binafsi. Usiogope kusema ukweli kuhusiana na kushinda na kushindwa kwako katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mmoja kuiishi changamoto kwa siku saba kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema kuwa atatupatia Roho mtakatifu atufundishe mambo yote (Yohana 14:26). Kwa ujasiri mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amfundishe kila mtu kuifanya changamoto.

# *Yohana 19:25-27*



# SURA YA SABA
# PENDA

***"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Yohana 13:35***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusaidia kutekeleza Changamoto ya Siku 7 kutoka katika sura iliyopita?"*

Akiwa amefunga taya zake na kuzibana kwa nguvu, mwanafunzi kijana alijilazimisha kumtazama Yesu alipokuwa anakufa. Saa kadhaa kabla mambo yalikuwa yanaonekana safi kabisa. Alikuwa akifurahia chakula cha jioni akiwa na Yesu, akikaa karibu kabisa Naye–mahali alipopapenda kukaa daima. Baada ya chakula cha jioni walikuwa wameenda safari ndefu pamoja hadi mlima wenye miti ya mizeituni. Ndipo jioni iliyokuwa njema kabisa iligeuka kuwa jinamizi la maisha yake.

Kundi la watu wakipepea hewani fimbo na marungu walimwagika katikati ya miti. Yuda kwa kujiamini alitangaza, "Ndiye Huyu!" Kundi la watu lilimkamata Yesu na kumfunga kamba. Wakiwa wamechanganyikiwa na wakiwa wameogopa, wanafunzi walimtelekeza Yesu na kumwacha mikononi mwa kundi la watu.

Yohana alitambaa kutoka kivuli hadi  kivuli akifuata kundi la watu kutoka umbali ulio salama walipokuwa nusu wakimwongoza, nusu wakimkokota Yesu kwenda mahakamani. Alipenya na kuingia chumba cha mahakama na akatazama Yesu akishitakiwa, akipigwa na akihukimiwa kifo. Alikuwa kimya. Sasa, akiwa amechelewa, alitamani kama angesema.

Alijikuta akiwa karibu na shina la msalaba. Je! Wanafunzi wengine wote walikuwa wapi? Alijua kwa nini yupo pale. Aliposikia Yesu akitoa maneno kwa kutweta, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui walitendalo," Yohana alitafakari yale ambayo Mwalimua alikuwa amemtendea.

Alikuwa mdogo kuliko wote, "Mtoto." Kulikuwa na tofauti kubwa kati yake na wanatimu wengine . Ilikuwa vigumu kwa yeyote kuelewa kwa nini Mwalimu alimwita amfuate.

Hakuja kwa mapendekezo ya mtu yeyote. Kila mtu alijua kuwa alikuwa na hasira kali. Alipochukizwa alijibu kwa kulipiza kisasi. Hakuna aliyejua ni wakati gani hasira yake ingelipuka. Kwa hiyo kundi halikuwa na upendo wa ziada kwake. Hakuna ambaye angesikitika ikiwa angekimbia na kurudi kwa mama yake.

Lakini Mwalimu alimpenda kana kwamba alikuwa mdogo Wake. Alisikiliza wakati wengine walimpuuza. Alitembea karibu naye.

Mwalimu alikwenda naye kila mahali. Na Kijana aliangalia, alisikiliza na alibadilika. Zaidi kuliko kingine chochote kile, alitaka awe kama Mwalimu alivyo. Upendo wa dhati wa Mwalimu ulimbadilisha  Kijana na kumfanya kuwa mtu ambaye anafanana sana na Mwalimu Mwenyewe. Sasa pale chini ya msalaba, Kijana  alimwangalia Mwalimu akikata roho. Machozi  yalitiririka chini kwenye mashavu yake wakati Yesu alipomwomba

amtunze mama Yake, Mariamu. Kijana  alisimama kando Yake wakati ilipoonekana kana kwamba ulimwengu wote ulimcheka Rafiki yake. Hakuna mtu aliyekuwa amewahi kumpenda, kumjali na kumwamini kama Yesu. Wakati huu asingeweza kukimbia.

Siku chache baadaye alikimbia kwenda katika kaburi lililo tupu. Aliishi maisha yake yote yaliyo baki kwa ajili ya Yule aliyempenda kuliko vitu vyote, Yesu, aliye hai, Mwokozi wa ulimwengu aliyefufuka. Miaka mingi baadaye,  "Kijana" aliandika Injili ya Yohana. Katika waraka huu, Yohana anajiita kwa kifupi tu kama "mmoja aliyependwa  na Yesu."

## Muda wa Mashauri

1. Taja watu watatu unaowapenda sana. Taja watu watatu katika maisha yako walio wagumu kuwapenda. Kwa nini unawapenda baadhi na unaona kuna ugumu kuwapenda wengine kuliko wengine?

2. Soma Yohana 13:35. Alama ya mwanafunzi wa Yesu ni nini?

3. Ikiwa wewe ni mdadisi, soma aya zifuatazo kuona jinsi Yesu alivyowekeza ndani ya Yohana: Mathayo 4:21; 17:1-13; Marko 5:37-43; 10:35-40; 13:3; 14:32, 33; Luka 9:49-56; 22:8; Yohana 19:26, 27

4. Katika maisha yako unawapendaje watu walio na matatizo? Soma Waefeso 4:29-32.

***Chagua mtu katika maisha yako ambaye anahitaji zaidi upendo wako.***

Jaribu kutumia hatua hizi zenye msaada:

(a) Waombee.

(b) Mwombe Mungu akupe upendo kwa ajili yao.

(c) Sema kile tu ambacho kinaweza kuwajenga kwa ukarimu na heshima.

(d) Salimisha uchungu wako wote kwa Mungu.

(e) Jitolee kuwabariki.

5. Kutatokea nini katika maisha yako ikiwa utaanza kumpenda kila mmoja kama Yesu anavyokupenda?

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Maisha ya Yesu yalimbadilisha "Kijana." Kila siku juma hili, chukua hatua mahususi kuwapenda watu wenye changamoto katika maisha yako**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 7

**Ukaribisho** (dak. 1) Mkaribishe kila mmoja mlangoni na msalimie kwa jina. Mfanye kila mmoja ajisikie kukaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ni nani amekuonesha upendo hata kama ulikuwa hustahili kupendwa?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililopita ukurasa wa 52:
*Yesu aliwatumikia wanafunzi Wake. Juma hili, tafuta njia mahususi kila siku kuwatumikia yatima, wajane, wageni, maskini, au yeyote aliye katika uhitaji.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, Mungu alikusaidiaje kuwatumikia walio katika uhitaji? Mwalike kila mmoja aunde timu na mwenzake ili kupata timu za watu wawili-wawili na kisha waulizane ikiwa waliitekeleza changamoto hiyo na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja kumtia moyo mwenzake hata kama hakufanya changamoto. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 kuongea miongoni mwa wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili ambao wanapenda kushiriki na kikundi chote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo kushoto mwa ukurasa wa 57. Uliza: Mbwa mwitu wanafurahisha sana kuwatazama. Ni kwa jinsi gani wanaonesha maneno ya Yesu katika Yohana 13:35? Jadili.

**Omba** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amtie moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo kila mmoja wa wana kikundi ataweza kujihisi kuwapo katika kisa husika! Fikiria kujumuisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

Muda wa Mashauri (dak. 20) Soma Neno. Jadilini maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 61. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto hii kwako wewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kushindi na kushindwa kwako katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu kuiishi changamoto katika siku saba zinazotangulia somo lijalo.

**Omba** (dak. 2) Ufanye wakati huu kuwa kilele cha somo hili. Mungu anasema kuwa tunda la Roho ni upendo (Wagalatia 5:22). Kwa ujasiri mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu akuze upendo Wake ndani ya kila mmoja anavyofanya changamoto hii.


Luka 24:13-32

# SURA YA NANE
# ISHI

***"...Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli." Yohana 8:31***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusaidia kutekeleza Changamoto ya Siku 7 kutoka katika sura iliyopita?"*

Wasafiri wawili wachovu walilinganisha notisi za mwisho wa juma. Waliamini kwa dhati kuwa Mwalimu alikuwa Yeye Yule aliyetabiriwa. Kukamatwa na kuuawa Kwake na wenye mamlaka viliwaacha katika giza la sonona. Jinsi gani jambo hili lingeweza kutokea?

Msafiri mwingine aliyekuwa peke Yake alijiunga nao. Hawakujali. Aliwauliza kile walichokuwa wakikijadili na alisikiliza kwa uvumilivu kisa chote. Walizungumzia kukatishwa tamaa kwao.

Rafiki yao aliwarejeza katika Maandiko waliyokuwa wameyasahau. Kipengele kwa kipengele Aliwafafanulia Neno Takatifu kwa shauku ambayo iliwaacha wale watu wawili bila pumzi. Aliwaonesha jinsi Mungu alivyokuwa ametabiri kuwa Masihi angekuja, angeishi, angekufa na kuingia katika utukufu Wake. Neno la Mungu lilileta uhai mpya katika giza la watu hawa waliokuwa wamekatishwa tamaa.

Wasafiri walisikiliza kwa umakini mkubwa. Walikuwa wamesikia Maandiko haya mara nyingi katika wakati uliopita. Unabii huu wa zamani ulikuwepo pale siku zote kwa ajili yao kuusoma, kuuamini na kuishi kwa huo kila siku.
Lakini hawakuwa wamefanyia kazi kile walichokuwa wamesikia. Walikuwa wamekosea maana ya msingi ya unabii huu.

Wawili hawa walipunguza kasi yao walipokaribia kijiji chao.  Nyumbani palikuwa karibu sana. Jua lilikuwa chini juu ya mashamba. Mgeni alianza kutembea Mwenyewe.

“Njoo nyumbani kwetu!” Walimwalika Mgeni. “Ni usiku sana kutembea Peke yako.” Mgeni alitabasamu Mwenyewe, aligeuka na kuenda nao nyumbani.

Chakula cha jioni kilikuwa na mambo mengi ya kushangaza. Mgeni aliinua juu mikono Yake ili abariki chakula. Hapo ndipo walipoona mikono Yake iliyotobolewa. Hapo ndipo walipoikumbuka sauti Yake. Yesu! Wataishi kwa Neno Lake milele!

## Muda wa Mashauri

1. Unaishi kwa kusikiliza maneno ya nani katika maisha Yako? Je, ni ya rafiki yako mpendwa? Mwenzi wako wa ndoa? Mfanyakazi mwenzako? Kwa nini unamsikiliza mtu huyo?

2. Soma Yohana 8:31, 32. Ina maana gani kukaa katika Neno la Yesu?

3. Soma Luka 24:13-35. Kwa jinsi gani Yesu alithamini Maandiko? Unawezaje kusoma na kutiii Neno la Mungu katika Maandiko? Vifuatavyo ni vidokezo vichache vya kusaidia:

***Yohana 5:39 Daima mfanye Yesu kuwa kiini cha kile unachokisoma. Jiulize mwenyewe, "Aya hii inanifundisha nini kumhusu Yesu?"***

(a) Yohana 16:13 Kabla ya kuanza kusoma, omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu ili awe Mwalimu wako

(b) Yakobo 2:17 Kabla ya kufunga Biblia yako, mwombe Mungu, "Nawezaje kutumia kile ninachojifunza katika maisha yangu?" Basi, nenda kafanyie mazoezi kile ambacho Mungu amekueleza kukitumia katika siku ya leo.

4. Ni badiliko gani linaweza kutokea katika maisha yako ikiwa utasoma Neno la Mungu na kuishi kwa Neno Lake kila siku?

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu anajifunua Mwenyewe kwako kupitia Neno Lake. Juma hili, lisome kila siku ili ufanye ugunduzi kumhusu Yesu na utumie ugunduzi huu kwa namna unavyoishi.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 8

**Ukaribisho** (dak. 1) Mkaribishe kila mmoja mlangoni na msalimie kwa jina lake. Mfanye kila mmoja ajisikie kuwa amekaribishwa na kuwa yeye ni sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ni kitu gani cha kwanza kinachokuja mawazoni mwako unapofikiria juu ya kitu kilichojaa uzima? Eleza katika maneno matatu, na angalia ikiwa kikundi kinaweza kubahatisha.

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililopita ukurasa wa 61:
*Maisha ya Yesu yalimbadilisha "Kijana." Juma hili, chukua hatua mahususi kila siku kuwapenda watu wenye changamoto katika maisha yako.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, Mungu alikusaidiaje kuwapenda watu wenye changamoto katika maisha yako?
Mwalike kila mtu kujiunga na mwenzake ili kuunda timu ya watu wawili-wawili na kila mmoja amwulize mwenzake ikiwa alifanya changamoto hiyo na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja kumtia moyo mwenzake hata kama kuna mmoja hajaifanyia kazi changamoto hiyo. Baada ya kutumia dakika 1-2 kujadiliana miongoni mwa watu wawili-wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja anapenda kushiriki uzoefu wake na kundi lote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo ukurasa wa 65. Uliza: Umeshaona shamba lililojaa alizeti? Kwa jinsi gani tendo lao la kuelekea upande wa jua wakati wa mchana huonesha kauli ya Yesu katika Yohana 8:31 kuhusu kukaa katika Neno Lake? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu atume Roho Mtakatifu kutia moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo kila mmoja atajiona yumo katika kisa hicho kwa wakati huo! Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi chako wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto ukurasa wa 68. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto hii katika maisha yako wewe mwenyewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kushinda au kushindwa katika kuiishi changamoto. Mpe kila mtu changamoto ya kuiishi changamoto kabla ya somo lijalo.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye wakati huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema kuwa Roho anatuongoza katika ukweli wote (Yohana 16:13). Kwa ujasiri mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amwongoze kila mtu katika ukweli wote wakati kila mmoja akiitekeleza changamoto hii.


Matendo 2:1-8

# SURA YA TISA
# NGOJA

***"Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba..." Matendo 1:4***

***Kabla hujaanza sura hii, tumia muda kujibu swali hili: "Mungu alikusaidiaje kutekeleza changamoto ya Siku 7 ya sura iliyotangulia?"***

Wakiwa wanaangalia juu kwenye anga angavu, wanafunzi walikaza macho kumwangalia Yesu akiinuka na kumezwa na msafara wa mawingu. Mwalimu alikuwa hai! Jambo lisiloweza kuaminika! Wanafunzi walijawa na furaha na mshangao.

Siku chache kabla walifikiria kila kitu kilikuwa kimepotea. Mwalimu wao alikuwa amekufa msalabani. Walikuwa wametumia mwisho wa juma wakiwa na hofu kuwa na wao wangekutwa na matatizo yayo hayo.

Kwa siku arobaini Mwalimu aliyefufuka alitembea na kuongea na wanafunzi Wake. Dhana ambazo zilionekana kuwa ngumu kabla ya ufufuo sasa zilieleweka kwao. Ndipo alipowakusanya pamoja katika mlima huu. Wanafunzi walikuwa na shauku ya kuuambia ulimwengu kuhusu Mwalimu wao.

Mwalimu wao alikuwa amewasamehe. Aliwapenda kiasi cha kutosha kuwapa changamoto ya kuwa vile alivyoona wangeweza kuwa. Walikuwa na maisha mapya, tumaini jipya na kusudi jipya kwa sababu Yake.

Walikuwa na shauku ya kwenda ulimwenguni kote wakiwa na habari hii, lakini Mwalimu alikuwa na neno moja kwa ajili yao, "Ngojeni." Aliwaambia waingoje ahadi waliyoahidiwa ya Roho Mtakatifu. Roho wa Mungu angewabadilisha na kuwasha moto usiozimika ndani yao wa kufanya wanafunzi kwa ajili ya Yesu!

Ilikuwa ni  vigumu kungojea. Roho zao zilikuwa zimejazwa upendo kwa ajili ya Mwalimu wao. Ilionekana kuwa jambo gumu kwao kurudi katika Chumba cha Juu kungoja na kuomba kwa ajili ya kile ambacho Mwalimu alikuwa ameahidi. Watu waliuliza, "Mnafanya nini huko juu katika chumba kile?" Waliweza kujibu, "Tunangoja."

Kwa siku kumi wanafunzi walingojea wakiwa katika Chumba cha Juu. Walipokuwa wakingoja, waliomba. Walipoomba, walitubu kila kitu kilichowazuia wasimpende Mwalimu na wasipendane wao kwa wao kikamilifu. Maadui waligeuka kuwa marafiki katika chumba. Waumini walifanyika ndugu. Wale ambao waliokuwa wakisengenyana wao kwa wao walifanyika kuwa ndugu na dada.  Fokasi ilikuwa kwa Yesu tu. Manung'uniko yalitoweka. Uchungu uliachwa.

Zawadi iliyoahidiwa haikuja mara moja. Kwa siku tisa hakuna kitu chochote kilichotokea kisichokuwa cha kawaida. Ahadi ya Mwalimu ilibaki bila kutimizwa.

Siku ya kumi, Roho Mtakatifu alimwaga uwepo Wake kwa nguvu mpya! Roho Mtakatifu aliunguruma katika chumba kama upepo wenye nguvu uendao kwa kasi. Kitu kilichoonekana kama ndimi za moto kilitulia juu ya kila mmoja.

Kila mtu alishikwa na njaa ya kuishi kwa ajili ya Yesu. Kila muumini alisikumwa kuwa mwaminifu kwa Mungu bila woga, bila kujali matokeo yake. Waliongea kwa nguvu yenye ushawishi iliyowafanya watu kusimama kwa ajili ya Yesu, kukimbia kutoka katika maridhiano hatarishi na kumfuata Yesu mahali popote, wakati wowote, kwa gharama yoyote.

## Muda wa Mashauri

1. Fikiria wakati ulipokuwa na kiu sana ya maji. Ungeweza kutoa nini kwa ajili ya kupata kinywaji ili kukata kiu? Kwa nini?

2. Soma Matendo 1:4, 5, 8 na 2:1-4, 8,11. Yesu aliahidi nini? Ni kitu gani kilitokea kama matokeo ya wanafunzi kungoja zawadi ya Roho Mtakatifu? Ni kitu gani Roho Mtakatifu aliwawezesha wanafunzi kukitangaza kwa lugha nyingi? (Tazama Matendo 2:8, 11.)

3. Utapokeaje karama hii ambayo Yesu aliiahidi? Jizoeze hatua hizi:

***Yohana 7:37-39–Mwamini Yesu na uwe na kiu zaidi kwa ajili Yake.***
***Matendo 2:38, 39–Tubu na ubatizwe.***
***Matendo 5:32–Mtii Mungu.***
***Luka 11:11-13–Mwombe Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu na mpokee kwa imani katika Neno la Mungu.***

4. Vipi ikiwa ungemwomba Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu akujaze kila siku? Maisha yako yangebadilikaje? Ninakualika umwombe Mungu kwa ajili zawadi hii.

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu anaahidi Roho Mtakatifu. Kila siku juma hili, mwombe Mungu akupe Roho Mtakatifu ili ayabadilishe maisha yako kila siku.**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura 9

**Ukaribu** (dak. 1) Mkaribishe kila mmoja mlangoni na umsalimie kwa jina lake. Mfanye kila mmoja ajisikie kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Eleza muda katika maisha yako ulipongoja kitu fulani, na ilikuwa jambo jema kusubiri.

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo lililoko ukurasa wa 68: *Yesu anajifunua Mwenyewe kwako kwa njia ya Neno Lako. Juma hili, isome kila siku ili kugundua kuhusu Yesu na kutumia ugunduzi huu kwa namna unavyoishi.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, ni ugunduzi gani ulioufanya kuhusu Yesu katika Neno Lake na ni kwa jinsi gani uliutumia ugunduzi huo?
Alika kila mmoja kujiunga na mwenzake na kuwafanya wote waunde vikundi vya watu wawili-wawili na waulizane wao kwa wao jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja awe anamtia moyo mwenzake hata kama kuna mtu hakuifanyia kazi changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja ametumia dakika 1-2 kuzungumza na mwenzake katika kikundi cha watu wawili-wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au wawili wanaotaka kushiriki na kundi zima.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo upande wa kushoto wa ukurasa 73. Uliza: Unafikiri huyu ndege kigong'ota anasubiri nini? Ndege huyu aitwaye kigong'ota anawakilishaje maneno ya Yesu ya Matendo 1:4? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amtie moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo wasikilizaji wako watajiona kuwa wapo pale kwa wakati huo! Fikiria kuwahusisha katika kikundi chako wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 76. Simulia kisa kutoka katika maisha yako kinachomaanishwa na changamoto katika maisha yako bianfsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kushinda na kushindwa kwako katika kuiishi changamoto. Mhamasishe kila mtu aende kuishi sawasawa na changamoto katika siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Fanya wakati huu kuwa kilele cha somo. Baba yetu wa mbinguni anaahidi kuwa Roho Mtakatifu atatupatia tunda Lake—upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi (Gal. 5:22-23). Omba kuwa kila mtu apokee zaidi tunda la Roho Mtakatifu wanapotekeleza changamoto ya juma hili.

# Matendo 8:25-39



# SURA YA KUMI
# MWANAFUNZI

***"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:18-20***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda kujibu swali hili: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusaidia kutekeleza changamoto ya siku 7 ya sura iliyopita?"*

Mawimbi ya joto yalimetameta. Vumbi lilitimuka na kupanda juu katika upepo wenye joto kali. Hapa palikuwa pahali pa mauti. Filipo alipitia upya maagizo ya malaika ya kutembea katika barabara ya jangwani. Kwa nini Mungu amtume katika mahali pale palipo ukiwa?

Filipo alipozunguka mwamba mkubwa usio na kitu ulioinuka juu, upepo ulitulia. Macho yake yalifungua. Bila kupenda aliruka aliposikia

midundo ya kwato zilizokuwa zikikaribia; gari la kukokotwa na farasi lilikuwa likikaribia. Ni nani, katika akili iliyo sawa, angeweza kuchagua kuja hapa?

Farasi wawili wazuri wa Kiarabu walikuwa wakikokota gari la kifahari lenye mapambo. Aliyekuwa amekaa katika gari alikuwa afisa kutoka katika ikulu ya Kandake, Malkia wa Ethiopia, akirudi kutoka kumwabudu Mungu katika mji wa Yerusalemu. Roho wa Mungu alimnong'onezea Filipi, "Nenda ukapande na gari lile."

Filipo alilikimbilia gari, alishangaa kusikia ofisa anasoma kutoka katika kitabu cha Nabii Isaya. "Unaelewa unachokisoma?" Filipo aliuliza. Ofisa alikunja uso wake, "Sawa, nawezaje kuelewa, bila mtu kuniongoza?" Anamwalika Filipo kupanda gari na kuungana naye.

Akishukuru kwa kupata fursa isiyotegemewa, Filipo anamfafanulia unabii ule ule uliokuwa umemduwaza ofisa, akimweleza mambo yote kumhusu Yesu. Wakiwa bega kwa bega, wakijifunza Maandiko, watu hao wawili wakawa ndugu katika imani.

Walipoendelea mbele, walikuta mahali kuna maji. Yule kiongozi akasema kwa sauti kubwa, "Angalia! Maji! Ni kitu gani kinanizuia nisibatizwe?" Filipo, akitabasamu, alimhakikishia kuwa angeweza kubatizwa ikiwa aliamini kikamilifu. Kwa dhati kabisa, Mkushi alipiga kelele, "Ninaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."

Gari la kukokotwa na farasi lilifunga breki na kisha kusimama. Wote wawili waliruka na kushuka chini na kuanza kutembea katika maji, ambapo Filipo alimzamisha ndani ya maji kama ishara ya kuzika njia zake za zamani na kujiweka wakfu kwa ajili ya kutembea katika maisha mapya katika Yesu. Wale watu wawili walitengana na Mkushi aliondoka na kuelekea nyumbani akimsifu Mungu kwa sauti kubwa–mwanafunzi mpya katika mahali pasipotegemewa!

## Muda wa Mashauri

1. Ni nani amekulea hadi ukafanya kitu ambacho kimekufanya uongeze thamani katika maisha yako?

***Kabla ya kufundisha ukweli mpya, mwulize mtu alichokifanya kwa kutumia ulichomfundisha wakati uliopita.***

2. Soma Mathayo 28:18-20. Yesu aliwapa wanafunzi Wake changamoto gani ya kufanya? Yesu ana mamlaka gani? Yesu alitoa ahadi gani kwa wale wanaofanya wanafunzi kwa ajili Yake?

3. Itakuwaje ikiwa kwa kukusudia kabisa utawafanya kuwa wanafunzi watu ambao Mungu amewaleta katika maisha yako? Orodhesha watu katika duara lako la ushawishi wasiomjua Yesu na maisha mapya Anayoyaleta.

Duara la ushawishi:

-
-
-

4. Kando ya kila jina, orodhesha mambo anayoyapenda na mahitaji ya mtu huyo katika maisha yake sasa.

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu anakutuma kwenda kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Kila siku juma hili, fuata uongozi wa Roho Mtakatifu, na uwe rafiki wa mtu mmoja.**

## Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 10

**Ukaribisho** (dak. 1) Kutana na kila mtu mlangoni na msalimie kwa jina lake. Mfanye kila mmoja kujisikia amekaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Fikiria kuwa umeshinda tiketi ya kutalii Antaktika. Kitu gani utakifanya kuwa cha kwanza katika orodha ya vitu vya kusafiri navyo?

**Swali** (dak. 5) Soma swali la changamoto la somo lililopo ukurasa wa 76:
*Yesu anakuahidi Roho Mtakatifu. Kila siku juma hili, mwombe Mungu akupe Roho Mtakatifu kila siku ili ayabadilishe maisha yako.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, Roho Mtakatifu alifanyaje kazi katika maisha yako?
Mwalike kila mmoja aungane na mtu mwingine na kuunda vikundi vya watu wawili-wawili na waulizane kila mmoja na mwenzake ikiwa kila mmoja wao aliifanya changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja amtie moyo mwenzake hata kama hakuifanyia kazi changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 kuongea na mwenzake kati ya wawili-wawili, uliza ikiwa mtu mmoja au wawili wanaweza kushiriki uzoefu wao na kundi zima.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyoko mkono wa kushoto wa ukurasa wa 81. Uliza: Paa anawafundisha nini watoto wake? Jambo hili linaelezeaje Mathayo 28:18-20? Jadili.

**Maombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kumtia moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo hadhira yako inaweza kujiona ikiwa sehemu ya simulizi hiyo kwa wakati huo!
Fikiria kuhusisha wengine katika kikundi chako wanaoweza kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 84. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua maana ya changamoto kwako wewe binafsi. Usiogope kusema ukweli kuhusiana na kushinda na kushindwa kwako katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mmoja kuiishi changamoto katika siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Fanya muda huu kuwa kilele cha somo. Mwombe Mungu kwa ujasiri amwimarishe kila mtu “kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani” ili kila mmoja aweze kufanya changamoto hii (Efe. 3:16).


Yohana 1:35-42;
6:1-14; 12:20-23

# SURA YA KUMI NA MOJA
# MWANAFUNZI-2

***“Tazama Mwanakondoo wa Mungu!”Sauti ya Yohana iliunguruma kama radi ikielekezwa kwa makutano ya watu wakati alipomtambua Yesu. Andrea aliinuka na kuangalia juu na kuacha kufungua viatu vyake. “Yohana alikuwa akimzungumzia nani?” alipatwa na mshangao mkubwa. Alikagua kundi la watu—watu maskini, watu matajiri na askari wakali wa Kirumi wakiwa wamesimama wima katika upepo mwanana wa asubuhi. Lakini alimwona mtu ambaye aliyeonekana kuwa mtu wa kawaida, fundi seremala, si chini ya hapo.***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: “Mungu alikusaidiaje kutekeleza changamoto ya sura iliyopita?”*

Fundi seremala alitembea taratibu akipita katikati ya kundi la watu waliokuwa wakiangalia kana kwamba hakuna jambo maalum lisilokuwa la kawaida lilikuwa limesemwa. Lakini kwa upande wa Andrea, tangazo la Yohana lilikuwa kitu ambacho moyo wake ulikuwa ukikitamani kwa muda mrefu kulisikia kwa kadiri alivyoweza kukumbuka. Hakusita. Ikiwa Yohana alikuwa amesema kuwa Masihi alikuwa amekuja, angemfuata!

Alitamani kuwa karibu na Yeye Aliyeahidiwa kwa kadiri iwezekanavyo. Yesu alimwonesha Andrea mahali Yeye alipoishi. Andrea alitumia siku nzima akiwa na Yesu, akitembea, akizungumza na akimega mkate pamoja na Yesu. Siku ile ilikuwa ni siku ya kwanza kati ya siku zaidi ya elfu moja za kutembea akiwa kando ya Yesu, akiishi kama Yesu alivyoishi.

Katika zile saa za kwanza, Andrea alijua kuwa Yesu angebadilisha maisha yake milele. Alikuwa amemgundua Masihi aliyetumainiwa! Asingeweza kubaki na habari hii njema yeye peke yake. Kwa vizazi vingi kila mmoja wa wananchi wake walikuwa wametumaini kumwona Masihi ambaye Mungu alimtuma kama mwanadamu. Ilimpasa kumwambia ndugu yake!

Andrea alitembea haraka-haraka, aliruka-ruka na halafu alikimbia kwa ndugu yake Petro. “Angewezaje kumshawishi ndugu yake Petro amfuate Yesu?” Je, angenukuu dondoo za unabii wa zamani? Je, awasilishe hoja zenye nguvu sana? Viatu vyake vilikanyaga ardhi akielekea nyumbani kwa Petro, mtumbwi wake, na maeneo aliyopendelea kukaa. Hatimaye alimpata Petro.

Andrea alifanya jambo muhimu sana kwa ajili ya ndugu yake: Alimleta Petro kwa Yesu! Andrea angeweza kumtuma kwa Yesu, lakini alichagua kwenda na Petro. Andrea alijitolea nafsi yake mwenyewe ili awe daraja la kumwunganisha Petro na Mwokozi!

Andrea aliona jinsi Yesu alivyobadili maisha yake mwenyewe. Alitazama miaka michache iliyofuata Yesu alivyobadili maisha ya kaka yake. Andrea aliona jinsi Yesu alivyomtia moyo Petro daima, alivyompa changamoto awafundishe wenzake. Yesu alitembea kwa uvumilivu pamoja na Petro siku hadi siku mpaka Petro akaanza kuakisi tabia ya Yesu Mwenyewe. Baada ya muda mrefu, Andrea alimwona Petro akibadilika kutoka kuwa mtu mwenye ubinafsi na asiyekuwa na uvumilivu hadi kuwa mtu mwenye upendo usiokuwa na ubinafsi na utu wema.

Andrea alipenda kuleta watu kwa Yesu! Siku moja wakati makutano walipokuwa wakimsikiliza Yesu walipopata njaa, Andrea alimwona mvulana mmoja mdogo akiwa na chakula cha mchana na akamleta kwa Yesu. Wakati baadhi ya Wagiriki walipokuja hekaluni wakimtafuta Yesu, Andrea mara moja aliwaunganisha hawa wageni na Mwokozi.

Hakuna hata mtu mmoja ambaye angeweza kusema Andrea alikuwa tofauti na wengine. Aliishi katika kivuli cha ndugu ambaye alimleta kwa Yesu. Aliishi nje ya duara la wale waliokuwa karibu zaidi na Yesu. Alimfuata tu Yesu popote pale Alipomwongoza kwenda na kwa kurudia rudia Andrea alileta watu aliokutana nao kwa Yeye Aliyekuwa amebadilisha maisha yake.

Andrea alikuwa mtu wa kawaida na asiyekuwa wa kushangaza, alikuwa mwaminifu kwa utume ambao Yesu alikuwa amempa kiasi ambacho alitokea kuwa mfano unaong'aa kwa wote ambao wangemfuata Yesu siku zote zilizofuata.

Andrea alionesha mfano wa Agizo la Injili: "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi..." (Mathayo 28:19)

Vipi kuhusu wewe? Utume wa Andrea ni utume wako, pia!

## Muda wa Mashauri

1. Fikiria watu katika maisha yako waliokutambulisha kwa mtu fulani ambaye walifikiria angeongeza thamani katika maisha yako.
   Ni nani alifanya jambo hili kwa ajili yako? Kwa nini walifanya hivyo?

2. Kufanya wanafunzi kwa ajili ya Yesu Kristo ni kuleta watu Kwake. Fokasi ni juu ya kuja karibu

na mtu na kujenga uhusiano wa kuaminiana. Ndipo unapoweza kumsaidia mtu huyo kuanza kumtumaini, kumfuata na kumshuhudia Yesu. Ni shughuli gani ambazo Yesu alizifanya kuwasaidia wakue katika safari yao ya imani? Tazama aya zifuatazo na orodhesha ugunduzi wako.

Mathayo 4:18-20

Mathayo 14:13-20 (hususani aya ya 16)

Mathayo 14:22-33

Luka 11:1-13

Yohana 13:5-15 (hususani aya ya 15)

3. Unawezaje kuchukua hatua inayofuata ili kumwunganisha mtu uliyemchagua katika sura ya 10 na Yesu?
Omba ili kujua hatua inayofaa.

***Shuhudia Yesu ni nani katika maisha yako na kile ambacho anakifanya kwa ajili yako.***

- Jitolee kuchunguza Biblia pamoja kila juma ili kugundua habari njema kumhusu Yesu.

- Mwombee mtu huyu kila siku. Uwe kielelezo kwa ajili ya ukweli ambao Mungu amekufundisha. Fundisha ukweli huu kutoka katika Maandiko.

- Mwalike mtu huyo kufanyia kazi kile ulichomfundisha na kukitumia katika maisha yake katika juma linalofuata.

4. Omba kwa dhati kwa ajili ya mtu huyu kila siku. Mwombe Roho Mtakatifu amtie moyo mtu huyu aishi kama mwanafunzi wa Yesu.

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu anakuvuta Kwake. Kila siku juma hili, mfuate Roho Mtakatifu amwunganishe rafiki yako na Kristo.**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 11

**Ukaribisho** (dak. 1) Kutana na kila mmoja mlangoni na msalimie kwa jina. Mfanye kila mmoja ajisikie kukaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ikiwa ungeweza kuishi mahali popote ulimwenguni, ingekuwa wapi na kwa nini?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya ukurasa wa 84: *Yesu anakutuma kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Kila siku juma hili, fuata uongozi wa Roho Mtakatifu, na uwe rafiki wa mtu fulani.*
Uliza: Katika siku saba zilizopita, Roho Mtakatifu alikusaidiaje kuwa rafiki wa mtu fulani?
Mwalike kila mmoja aungane na mtu mwingine ili kuunda timu za watu wawili-wawili na waulizane ikiwa walifanya changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja kumtia moyo mwingine hata kama kuna mtu hakufanya changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 kutoa ushuhuda wakiwa katika makundi ya watu wawili-wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili ambao wangependa kushiriki na kikundi chote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyopo upande wa kushoto wa ukurasa wa 89. Uliza: Jadili. Kereng'ende wanakamataje chakula chao? Wanatukumbushaje ahadi ya Yesu iliyopo katika Mathayo 4:19?

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu kufariji kila moyo.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo hadhira yako inaweza kujiona kuwa pale katika muda huo! Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi wanaopenda kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno.  Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa wa 93. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua kile ambacho changamoto hiyo inamaanisha katika maisha yako wewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kushinda au kupoteza katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu aiishi changamoto hiyo katika siku saba zinazofuata kabla ya somo lijalo.

**Ombi** (dak. 2) Ufanye muda huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema kuwa Roho Mtakatifu anatusaidia kusema (Mathayo 10:19, 20). Kwa ujasiri mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amsaidie kila mmoja kusema wakati anapofanya changamoto hii.



## *Matendo 4:36, 37; 9:1-31; 11:19-26*

# SURA YA KUMI NA MBILI
# MWANAFUNZI-3

***"Tazama Mwanakondoo wa Mungu!"Sauti ya Yohana iliunguruma kama radi ikielekezwa kwa makutano ya watu wakati alipomtambua Yesu. Andrea aliinuka na kuangalia juu na kuacha kufungua viatu vyake. "Yohana alikuwa akimzungumzia nani?" alipatwa na mshangao mkubwa. Alikagua kundi la watu—watu maskini, watu matajiri, na maaskari wakali wa Kirumi wakiwa wamesimama wima katika upepo mwanana wa asubuhi. Lakini alimwona mtu ambaye aliyeonekana kuwa mtu wa kawaida, fundi seremala, si chini ya hapo.***

*Kabla ya kuanza sura hii, tumia muda mfupi kujibu swali hili: "Mungu alikusaidiaje kutekeleza changamoto ya Siku ya Saba?"*

Jasho lilitiririka katika shingo ya Barnaba licha ya usiku wenye baridi. Je, alikuwa karibu kusaliti wafuasi wa Yesu kwa mwuaji kichaa? Alishangaa. Kwa kusitasita alimwongoza Sauli wa Tarso na kumpeleka katika mkutano wa siri ambapo Yakobo na wanafunzi wengine wa Yesu walipafanya kuwa chumba cha kila siku cha makao makuu ya kanisa la awali.

Barnaba alipunguza hatua zake. Kwa hatua za kukosa uhakika, Sauli alionesha kusita pia. Mbele yao katika uchochoro mwembamba kulikuwa na mlango mkubwa, wenye makovu. Alijua mfululizo wa ugongaji mlango ambao ungeashiria wanafunzi walioko ndani kuwa wangeweza kufungua mlango katika hali ya usalama. Alikuwa akichukua hatua ya hatari sana?

Barnaba mwenyewe binafsi aliwajua wengi wa wale aliokuwa amewatia gerezani na wale ambao alikuwa amewaua, lakini aliamini pia kuwa Yesu Kristo alikuwa amekutana na Sauli nje ya mji wa Dameski. Sasa Sauli alikuwa amebadilishwa kwa neema na upendo wa Yesu. Chuki ya Sauli kwa Mwokozi ilikuwa imeondoka na mahali pake upendo ulichukua nafasi ambayo ilimsukuma kumweleza kila mmoja aliyekutana naye juu ya nguvu ya Yesu inayobadili maisha.

Barnaba alibisha hodi na mlango mchakavu wa zamani ulifunguka. Wanafunzi wa Yesu walitazama wakiwa kimya, wakati Barnaba alipomwongoza Sauli hadi katikati yao. Barnaba aliinua mikono yake juu na kusitisha dhoruba ya maswali na mashtaka, na ndipo alipowaomba wanafunzi wamkubali Sauli kama mmoja wao. Machozi yalibubujika kutoka katika macho yao waliposikiliza kwa mshangao kisa cha neema ya Mungu kwa ajili ya mwanafunzi huyu wa Yesu aliyekuwa hatarajiwi sana.

Wanafunzi kwa tahadhari, halafu kwa furaha walimkumbatia mtesaji wao wa zamani. Sauli alilia.

Kwa sababu Barnaba alimwamini Sauli, uongozi wa kanisa ulimkubali Sauli. Barnaba alihatarisha maisha yake kwa kumleta Sauli kwao, kwa hiyo walihatarisha maisha yao kwa kumpokea. Mtu fulani anahitaji daima kujenga daraja kwa ajili ya mtu mwenye changamoto. Barnaba alikuwa mtu huyo.

Lakini Barnaba hakuishia kumtambulisha Sauli tu. Baadaye alisafiri kwenda Tarso kumtafuta Sauli. Alipompata, Barnaba alimchukua Sauli hadi Antiokia na kufanya kazi naye pale kwa mwaka mmoja.

Barnaba alijua kuwa Mungu alikuwa amembadilisha Sauli kwa njia ya nguvu ya Roho Mtakatifu. Alijua pia kuwa Sauli alihitaji kufanywa mwanafunzi. Barnaba alitumia muda kujenga uhusiano na Sauli. Alimkaribisha Sauli katika maisha yake.

Kwa mwaka mzima Sauli alikuwa na faida ya kutembea na mwumini huyu kwa muda mrefu. Sauli aliweza kuona jinsi Barnaba alivyoishi kwa kumwamini Yesu. Alimwona Barnaba akiomba, akisoma Neno la Mungu, akifanya urafiki, na akiufanya mji umfuate. Aliweza kuona jinsi Yesu alivyobadili njia ambayo Barnaba alifanya kazi na waumini na jamii ya wasioamini.

Katika miezi iliyofuata Barnaba alimfanya Sauli kuwa mwanafunzi. Barnaba hakuishia tu kumwambia Sauli Injili; aliiishi na kila siku alimwalika Sauli kujiunga naye katika safari ya kumfuata Yesu!

Alimwalika Sauli kujiunga naye alipofundisha Neno la Mungu, alipohubiri kutoka nyumba kwa nyumba, katika masinagogi, na nje katika mvua, katika joto na katika baridi. Sauli alimwangalia Barnaba akiwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi na akifanya kazi na waumini wa zamani. Barnaba kwa uvumilivu mwingi alimtia moyo Sauli alipokuwa akijifunza kuwa kama yeye.

Barnaba alianza kutambua kuwa makutano walianza kuja kumsikiliza Sauli, siyo yeye tena. Barnaba aliangalia kwa kicho wakati Roho Mtakatifu akimwezesha Sauli kuhubiri habari njema ya Yesu kwa wanaume na wanawake wenye mvuto mkubwa na uwezo mwingi. Alitazama wakati watu walipovutwa kwa nguvu kwa Kristo. Barnaba mfanya wanafunzi kimya kimya alibadilika kutoka kuwa mlezi na kuwa mwenza na baadaye kuwa msaidizi aliyesahauliwa mara kwa mara.

Roho Mtakatifu wa Mungu alimbadilisha Sauli na kumfanya kuwa Paulo mtume pendwa. Kwa kurudia-rudia Paulo alirudi katika miji mahali

ambapo yeye na Barnaba walihubiri kwanza Injili na kuwatia moyo wanafunziili kuwaleta maelfu kwa Yesu.

Mungu atakuongoza kwa wanafunzi wengi wasiotarajiwa kwa ajili ya Kristo. Tumia muda. Hatarisha maisha yako. Wekeza maisha yako katika kufanya wanafunzi kwa ajili ya Kristo wanaomwamini, wanaomfuata na kumshiriki Yesu kwa wengine wakati wowote, mahali popote, na kwa gharama yoyote. Pata uzoefu wa furaha ya kumwona Mungu akiwatumia hawa wanafunzi kuwaandaa watu kukutana na Kristo anayekuja upesi!

Uwe Barnaba! Nenda ukafanye wanafunzi!

## Muda wa Mashauri

> ***Tambua mtu aliyeamini kuwa una thamani ingawa wengine hawakuona kuwa una thamani. Kwa nini aliwekeza katika maisha yako?***

1. Je, una mtu fulani katika familia yako, duara la marafiki, shule, au mahali pa kazi anayeonekana kama mwanafunzi asiyetarajiwa? Omba kuwa Mungu akusaidie kuona kile ambacho Mungu anakiona ndani yao.

2. Soma Matendo 9:1-8, 19-22, 26-28; 11:22-26. Andika orodha ya hatua ambazo Barnaba alizichukua kumsaidia Sauli kukua kama mwanafunzi na mfanya wanafunzi wa wengine.

3. Unapokutana tena na mtu uliyeanza kumfanya mwanafunzi juma lililopita, mwulize mtu yule alichokifanya kutokana na kile ulichomfundisha. Sherehekea popote pale wanapotumia ukweli wa Neno la Mungu. Uwe mvumilivu wanapopambana au wanaposahau. Mungu ni mwenye rehema! Wasaidie kugundua kile ambacho inawezekana Mungu anawaita kukifanya wakati ujao.

4. Unapoamini kuwa mtu yule anaishi na kutumia ukweli mahususi uliomfundisha, mpe changamoto ya kushiriki ukweli huo na mtu mwingine. Kumbuka kuwa Mungu anawabadilisha watu kwa kasi tofauti. Uwe mvumilivu. Kama vile ambavyo Mungu amekuvumilia na wewe, chukua muda kufurahia safari kwa kadiri jinsi Mungu anavyombadilisha mtu unayemfanya kuwa mwanafunzi.

5. Unapomwona huyo mtu tena, mwulize mambo yalikwendaje aliposhiriki imani yake na mtu mwingine. Tena, sherehekea mafanikio ambayo Mungu aliyatoa na mtie moyo kwa changamoto anazokutana nazo. Mwombe Mungu amwoneshe kile ambacho Mungu anataka mtu huyo akifanye muda mwingine ujao.

## CHANGAMOTO YA SIKU 7

**Yesu anawekeza maisha Yake kwako. Juma hili, wekeza maisha yako kwa mtu ambaye Roho Mtakatifu amekuita kumfanya kuwa mwanafunzi.**

# Mwongozo wa Kikundi Kidogo kwa ajili ya Sura ya 12

**Ukaribisho** (dak. 1) Kutana na kila mtu mlangoni na kumsalimu kwa jina lake. Mfanye kila mmoja ajisikie kukaribishwa na kuwa sehemu ya kikundi.

**Kuvunja Ukimya** (dak. 8) Uliza: Ikiwa ungekuwa mnyama wa aina yoyote, angekuwa mnyama gani? Kwa nini?

**Swali** (dak. 5) Soma changamoto ya somo la mwisho iliyoko ukurasa wa 93:
*Yesu anatuvuta Kwake. Kila siku juma hili, mfuate Roho Mtakatifu amuunganishe rafiki yako mpya kwa Kristo.*
Uliza: Katika siku saba za mwisho, kwa jinsi gani Roho Mtakatifu alikusaidia kumwunganisha rafiki yako mpya na Kristo?
Mwalike kila mmoja akae na mtu mwingine ili kuunda timu ya watu wawili-wawili na waulizane katika kila kikundi ikiwa walifanya changamoto na jinsi mambo yalivyokwenda. Mkumbushe kila mmoja kumtia moyo mwenzake hata kama mtu mmojawapo hajaifanya changamoto hiyo. Baada ya kila mmoja kutumia dakika 1-2 za kujadiliana katika vikundi vya watu wawili-wawili, uliza ikiwa kuna mtu mmoja au watu wawili ambao wanapenda kushiriki uzoefu wao na kikundi chote.

**Picha** (dak. 3) Onesha picha iliyoko upande wa kushoto wa ukurasa wa 97. Uliza: Je, shakwe mkubwa anaweza kuwa anamfanyia nini shakwe mdogo? Mfano huo unawakilisha kitu gani Barnaba alichomfanyia Sauli katika Matendo 11:25-36? Jadili.

**Ombi** (dak. 1) Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amtie moyo kila mmoja.

**Kisa** (dak. 5) Soma kisa kwa namna ambayo hadhira itajisikia kuwa pale kwa muda huo! Fikiria kuwahusisha wengine katika kikundi chako ambao wangependa kusoma.

**Muda wa Mashauri** (dak. 20) Soma Neno. Jadili maswali.

**Changamoto** (dak. 5) Soma changamoto iliyopo ukurasa 102. Simulia kisa kifupi kutoka katika maisha yako kinachofunua kile ambacho changamoto hii inamaanisha kwako wewe binafsi. Usiogope kuwa mkweli kuhusiana na kufanikiwa au kushindwa katika kuiishi changamoto. Mpe changamoto kila mtu kuiishi changamoto hiyo kwa siku saba zijazo kabla ya somo linalofuata.

**Ombi** (dak. 2) Fanya muda huu kuwa kilele cha somo. Mungu anasema kuwa ninyi wanafunzi Wake mtapokea nguvu atakapowajilia Roho Mtakatifu juu yenu (Matendo 1:8). Kwa ujasiri mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu amsaidie kila mmoja kuifanya changamoto hii kwa nguvu Zake!

# CHANGAMOTO YANGU KWAKO

Je! Utafanya nini ukiwa na Yesu? Utazingatia, lakini usijisalimishe? Utafurahia harufu ya upendo Wake, lakini ukatae kutumwa? Utafurahia urafiki huu, halafu uache kumfuata?

Nimemjua Yesu kwa karibu nusu karne. Nimesoma sana kumhusu Yeye katika Neno Lake na nimekuwa na furaha katika kudai kuwa mfuasi Wake. Natafakari upya maisha yangu na ninajikuta nikiwa na shukrani kwa ajili ya huruma Yake na utunzaji Wake kwa miaka mingi—na bado ninahuzunika kwa nyakati nyingi ambazo nilimfuata Yesu nusu nusu, au hata sehemu kubwa na njia, lakini siyo njia yote. Ananiita mimi na wewe kufanya mambo makubwa zaidi!

Yesu alitembea juu ya sayari hii kwa nyayo Zake Mwenyewe. Anajua mapambano yetu. Anajua hofu zetu. Anajua mielekeo yetu ya kurudi nyuma, kutafuta kilicho salama, na kugeuka kwenda mbali na kafara. Anatujua sana na jinsi ya kugeuza kushindwa kwetu kuwa kufanikiwa kwa neema Yake yenye nguvu.

Niko magotini wakati huu sasa, ninapomwaga moyo wangu wote kwako. Hiki ndicho ambacho Mungu amenielekeza kukuambia:

1. Ishi kila wakati ukijua kuwa Mungu anakupenda milele! Tazama Warumi 8:38, 39.

2. Jisalimishe kikamilifu kwa Mungu kila siku, ukimpatia kila kitu, ukimpa vyote ulivyo na kila kitu ulicho nacho kitumiwe kuleta utukufu mkuu wa Yesu. Tazama 1 Wakorintho 10:31.

3. Soma Neno la Mungu kwa uaminifu na ukiwa na lengo la kubadilisha maisha yako kulingana na kile unachokisoma katika siku ile. Ishi kile unachokisoma. Jaribu kila kitu unachokiamini na kukiishi kwa Neno Lake. Tazama 2 Timotheo 3:15-17.

4. Tumia muda usiokuwa na haraka kuzungumza na Mungu na kusikiliza sauti Yake ndogo ya upole. Zipe changamoto tafsiri zako za kile ulichokisikia kwa Mungu kwa kutumia Neno la Mungu lililoandikwa. Tazama Zaburi 5:3; 46:10; 1 Wafalme 19.

5. Uwe na uhakika wa wokovu kwa njia ya neema ya Yesu pekee. Tazama Waefeso 2:8, 9.

6. Ombea kupata ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu ili Mungu akuze tabia yako hadi iwe kama ya Yesu na akupe kutokuwa na hofu katika kumshuhudia Yeye kwa mtu yeyote. Tazama Matendo 1:4, 5.

7. Waume, wapendeni wake zenu kwa kujitoa mhanga, kama Yesu alivyokupenda. Wake, waheshimuni waume zenu. Watauona upendo wa Yesu katika namna mnavyowaheshimu. Tazama Waefeso 5:25, 33.

8. Mwaga maisha yenu katika kuwafanya watoto wenu kuwa wanafunzi wa Yesu. Huu ni wito wenu. Usimpe mtu mwingine dhamana hii nje ya nyumba yako. Watu wengine wanaweza kusaidia kazi yako, lakini kamwe hawawezi, kabisa kuchukua nafasi ya kile ambacho Mungu amekuita kukitoa wewe mwenyewe kwa watoto wako. Ikiwa huna watoto wako mwenyewe, tafuta njia ya kuwekeza maisha

yako kusaidia kizazi kinachofuata wawe wanafunzi wa Yesu. Tazama Kumbukumbu 6:4-9; Malaki 4:5, 6; Matendo 2:17.

9. Shiriki kile unachokigundua kila siku katika Neno la Mungu na mtu mwingine. Lakini usiishie tu kushiriki Neno. Wekeza maisha yako katika kumsaidia mtu mwingine awe mwanafunzi wa Yesu ili wapate furaha ya kuamini, kufuata na kumshuhudia Yesu! Tazama Mathayo 28:18-20.

10. Tafuta ndoto zako ulizopewa na Mungu, mipango ile ambayo Mungu alikuwa nayo kwa ajili ya maisha yako kabla hujazaliwa. Mtumikie kwa uaminifu mahali popote ulipo, lakini mfuate popote anapokuita na kukutuma wakati wowote, mahali popote, na kwa gharama yoyote. Mtumikie Mungu kwa umuhimu na uharaka wa kurudi kwa Yesu! Tazama Yeremia 1:5; Zaburi 139; Waefeso 3:20, 21; 1 Wathesalonike 4:16-18.

Mungu akubariki unapomfuata Yesu!

Ndugu yako katika Yesu,

Don

# Uongozi wa Kikundi Kidogo

1. Mwombe Mungu akusaidie kufikiria watu wanaopaswa kunufaika kwa kujiunga na kikundi kuchunguza namna ya kuishi kama mwanafunzi wa Yesu.

2. Waombee wale unaovutwa kuwaalika kuja katika kikundi.

3. Alika rafiki zako, majirani zako, wanadarasa wenzako au wafanyakazi wenzako waje nyumbani kwako au mahali pengine popote pale panapofaa kwa ajili ya kikundi chako. Waalike waje na kupata uzoefu wa mkutano mmoja.

4. Ikiwa wataona wamepata manufaa, watie moyo warudi kwa ajili ya mikutano kumi na mbili inayofuata. (Sura ya nne inagawanyika vizuri zaidi katika majuma mawili.)

5. Fikiria kutoa mlo rahisi kabla ya mkutano wa kikundi kidogo au vinyaji vya baridi baada ya mkutano. Watu daima wanatafuta urafiki wa kweli kama huu. Chakula kinaweza kisiwe sehemu ya uzoefu wa kikundi kidogo, lakini mara nyingi ilikuwa sehemu ya uzoefu wa ufanyaji wa wanafunzi katika karne ya kwanza.

6. Muundo pendekezwa wa Mkutano wa Kikundi Kidogo:

   A. Mkaribishe kila mtu kila mnapokutana kila juma. Fungua kwa swali kama vile: “Ni neno gani linaeleza vizuri wiki yako?” Tumia muda mfupi kwa ajili ya

wajumbe wa kikundi chako kushiriki kile kinachotokea katika maisha yao. Ukimwalika kila mtu kushiriki na mwenzake kutaokoa muda na kuwatia moyo wale ambao wana aibu.

B. Baada ya juma la kwanza, daima alika kikundi kutolea ushuhuda kile ambacho kila mmoja alikifanya katika kutekeleza "Changamoto ya Siku 7" iliyotolewa juma lililopita. Zoezi hili linakuwa zuri zaidi likifanywa katika vikundi vya watu wawili-wawili. Fundisha wana kikundi kuulizana kila mmoja na mwenzake, "Mambo yalikwendaje katika kutekeleza changamoto katika juma lililopita?" Suala ni kuwa mtiane moyo na mtegemezane katika kuchukua hatua za imani na kutegemezana katika kuchukua hatua ambazo Mungu anataka tuzifuate. Watie moyo wanakikundi waulize kwa upendo na neema, kwa sababu mtu hawezi kujua matatizo ambayo mtu mwingine anayopitia katika kuchukua hatua ya imani ya kumfuata Yesu.

C. Mwombe Mungu alibariki kundi na Neno Lake lililoandikwa unapokuwa ukisoma na kulitumia.

D. Kialike kikundi kujifunza picha na aya ya Biblia inayofungua sura. Waombe watoe maoni yao juu ya jinsi asili inavyoonesha kielelezo cha aya.

E. Uliza wote wale walio tayari kusoma paragrafu ya historia.

F. Endelea na muda wa mashauri katika namna ile ile—ukihusisha kikundi katika kusoma maswali na aya za Biblia. Alika kikundi kushiriki maoni yao.

G. Mara tu baada ya kusoma Changamoto ya Siku, eleza kile ambacho changamoto hiyo humaanisha katika maisha yako na jinsi ambavyo Mungu anakuongoza kutekeleza hatua hii katika kumfuata Yesu. Mwombe Bwana akupatie ushuhuda ambao hautafaa tu kwa ajili ya changamoto, bali pia utafaa kwa ajili ya wanakikundi. Mungu anajua kile ambacho wanakikundi hicho wanahitaji kukisikia na ambacho kitagusa mioyo yao. Hakikisha kuwa unakifanya kuwa kifupi na rahisi na juu ya yote, kiwe halisi.
Kumbuka kuwa unajifunza na kukua sawa na mwingine yeyote yule. Utagundua kuwa ikiwa uko radhi kujihatarisha katika kushiriki jinsi changamoto hiyo inavyokugusa, basi utamtia moyo kila mwanakikundi kufanya hivyo pia.

H. Hakikisha kuwa kila hatua katika kumfuata Yesu iko wazi kwa kikundi. Kumbusha kikundi kuwa hatua itaonekana tofauti katika mazingira ya kila mtu.

I. Funga kwa ombi la baraka. Kwa kadiri kikundi kinavyoendelea kukua na kuwa karibu kwa pamoja, watakuwa na mambo ya kuombea. Tumia muda kuuliza na kusikiliza.

J. Jipange kuwa karibu kwa ajili ya wale walio na maswali au wanaoweza kuhitaji kutiwa moyo kumfuata Yesu.

K. Mtie moyo kila mmoja ajiweke wakfu kuwa katika kikundi kidogo kilichojitolea kumfuata Yesu. Kujitolea huku kutatiwa moyo kama njia ya maisha.

6. Daima mhamasishe mmoja wa wana kikundi aongoze kikundi kidogo pamoja na wewe. Omba kwa ajili ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Atakusaidia. Mpe mtu huyu jukumu kila juma la kuongoza. Anza na mambo madogo anayoweza kusaidia katika kuongoza na umwongeze majukumu ya uongozi kwa kadiri unavyoona Mungu akimkuza.

7. Omba kwa ajili ya washiriki wa kikundi chako kidogo kila siku. Mwombe Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu ambadilishe kabisa kila mmoja wao wanapokuwa wakimfuata Yesu.

# FUATA

WAKATI WOWOTE, MAHALI POPOTE,
KWA GHARAMA YOYOTE

Umepata kitu chochote kizuri sana kiasi kwamba unaweza kwenda wakati wowote, mahali popote kwa gharama yoyote kwa ajili ya kukipenda? Kulikuwepo harakati za watu katika karne ya kwanza waliopata kitu kizuri. Walimpata Yesu na walitetemeka sana walipojua kuwa mtu yeyote angeweza kuwapenda sana kiasi kile! Wafuasi hawa wa Yesu wa awali waliupindua ulimwengu wao kichwa chini miguu juu walipoishi maisha yaliyobadilika. Amani katika nyuso zao, upendo wa wazi katika familia zao na nguvu itoayo uzima ya maisha yao iliwasukuma rafiki zao kukitaka kile walichokuwa wamekigundua.

Fuata kinakufundisha katika safari yako ya kukua kama mfuasi wa Yesu wa karne ya 21! Miaka elfu mbili imepita tangu Yesu atembee juu ya sayari hii. Sehemu kubwa ya ulimwengu imesahau furaha, amani na kusudi ambalo Mwalimu kutoka Galilaya alivileta kwa watoto, vijana na watu wazima miaka mingi iliyopita. Ni wakati wa kugundua upya maana ya kumfuata!

Kugundua masomo yenye msaada zaidi kwa ajili yako na familia yako, tembelea tovuti ya www.InDiscipleship.org.



Don na bibi arusi wake April huishi katika nyumba inayozungukwa na miti na mashamba yenye ukimya ya Apison, Tennessee. Kwa zaidi ya miaka 35, wamekuwa na furaha ya kumfuata Yesu wakiwa pamoja."